# Kiswahili

## Kwa vyuo vya Ualimu

### MWONGOZO WA MKUFUNZI

2

MICHEPUO: ECLPE, SME & SSE

© 2020 Bodi ya Rwanda ya Elimu ya Msingi

Haki zote zimehifadhiwa.

Kitabu hiki ni mali ya Bodi ya Rwanda ya Elimu ya Msingi.

Shukrani lazima zitolewe kwa Bodi ya Rwanda ya Elimu ya Msingi wakati yaliyomo yamenukuliwa.

# VIFUPISHO

***n.k***: *na kadhalika*

***k.v***: *kama vile*

***tnbh***: *tanbihi*

***m.f***: *mfano*

***agh***:*aghalabu*

***Bi.*** : *Bibi*

***Bw.*** : *Bwana*

# DIBAJI

**Mkufunzi mpendwa,**

Bodi ya Rwanda ya Elimu ya Msingi inayo heshima kwa kutoa kitabu hiki cha Kiswahili cha mwongozo wa mkufunzi kwa wanafunzi wa mwaka wa pili michepuo mingine. Kitabu hiki ni waraka rasmi utakaoongoza ufundishaji na ujifunzaji kuendana na mtaala uegemeao katika uwezo. Falsafa ya elimu Rwanda inalenga katika kumpatia mlengwa uwezo katika kila ngazi ya elimu ili kuweza kumudu vizuri katika jamii na kumpa fursa ya kujipatia ajira.

Ili kwenda sambamba na juhudi za kuboresha elimu, Serikali ya Rwanda inasisitiza umuhimu wa kufungamanisha ujifunzaji na ufundishaji na zana pamoja na mitaala ili kuwezesha mchakato wa ujifunzaji. Mambo mengi huathiri yale ambayo wanafunzi wanafundishwa, namna nzuri ya kujifunza na uwezo waupatao. Mambo hayo ni pamoja na umuhimu mahususi wa yaliyomo,ubora wa wakufunzi, mbinu za ufundishaji na ujifunzaji, mikakati ya upimaji na vifaa vya kufundishia vilivyopo.

Tumezingatia umuhimu wa mbinu zenye mchakato wa kujifunza ambao unamwezesha mwanafunzi kuendeleza mawazo yake na kufanya ugunduzi mpya wakati wa mazoezi thabiti yawe ya binafsi au katika makundi, kwa msaada wa wakufunzi ambao majukumu yao ni kufanikisha ufundishaji. Watapata stadi za lugha zinazofaa zitakazowawezesha kutumia yale waliyojifunza katika miktadha ya maisha halisi. Kwa kufanya hivyo, wataonyesha tofauti siyo tu katika maisha yawo bali hata kwa taifa .

Hii inatofautiana na mfumo wa zamani kuhusu nadharia ya ujifunzaji iliyosisitiza mchakato wa kujifunza kama upataji wa maarifa kutoka kwa yule aliyemzidi maarifa na hasa akiwa ni mkufunzi.

Katika mtaala uegemeao katika uwezo, ujifunzaji unachukuliwa kama mchakato wa kazi ya kujenga na kuendeleza maarifa na ufahamu, stadi na maadili na mwenendo mwema kutoka kwa mwanafunzi ambapo dhana aghalabu huanzishwa kwa mazoezi, hali na mazingira yanayomsaidia mwanafunzi kujenga maarifa, kuendeleza stadi na upatikanaji chanya wa maadili na mwenendo mwema.

Aidha, kazi ya kujifunza hujishughulisha na wanafunzi kwa kufanya mambo na kufikiri kuhusu yale wanayoyafanya na wanafarijika kuonyesha uzoefu wao halisi na maarifa katika mchakato wa ujifunzaji.

Katika mtazamo huu jukumu lako litakuwa :

- Kuandaa masomo yako na vifaa vya ufundishaji vinavyofaa,
- Kuandaa majadiliano katika makundi ya ushirikano kwa wanafunzi ukizingatia umuhimu wa ushauri kuwa kujifunza hufanyika kwa ufanisi wakati mwanafunzi afanyapo kazi kwa kushirikiana na watu wanaomzidi maarifa na uzoefu,

- Kuwashirikisha wanafunzi kwa kupitia kazi za ujifunzaji kama: njia ya uchunguzi, makundi ya mijadala, utafiti, mazoezi ya utafiti na kazi za kibinafsi,
- Kutoa fursa ya usimamizi kwa wanafunzi kwa kuendeleza uwezo wao, kwa kuwapa ushindani tofauti na kutoa majukumu yanayoongeza tafakuri tunduizi, utatuzi wa matatazo, ubunifu na uvumbuzi, mawasiliano na ushirikiano,
- Kutoa msaada na kuwezesha mchakato wa ujifunzaji kwa kutathmini mchango wa wanafunzi katika mazoezi ya darasani,
- Kuwaongoza wanafunzi ili waweze kuoanisha matokeo ya utafiti,
- Kutilia maanani tathmini ya kazi binafsi na kazi za makundi zilizofanyika darasani kwa kutumia mchakato na mbinu zinazoegemea katika uwezo wa wanafunzi,
- Kwa kukusaidia katika kazi yako ya kufundisha, yaliyomo katika mwongozo huu wa mkufunzi yanaeleweka kiasi kwamba unaweza kutumiwa kwa urahisi.

Mwongozo huu umegawanyika katika sehemu tatu (3)

**Sehemu ya 1:** Inaelezea muundo wa kitabu hiki na kukupa mbinu na maelekezo ya ufundishaji.

**Sehemu ya 2:** Inakupa sampuli ya andalio la somo kama marejeleo ya mchakato wa kuandaa somo.

**Sehemu ya 3:** Inatoa mwongozo au maelekezo ya ufundishaji kwa kila dhana iliyotolewa katika kitabu cha mwanafunzi.

Ingawa mwongozo huu wamkufunzi una majibu kwa kila kazi zote zilizotolewa katika kitabu cha mwanafunzi, unaombwa kupitia kila swali na kazi kabla ya kutathmini matokeo ya utafiti.

Napenda kwa moyo wote kutoa shukrani zangu kwa watu wote walioshiriki kutoa mchango wao wa kuboresha mwongozo huu wa mkufunzi, na hasa wafanyakazi wa Bodi ya Rwanda ya Elimu ya Msingi ( REB/CTLR) walioandaa mchakato wa kazi hii tokea ilipoanzishwa.

Pongezi maalum ziwaendee wakufunzi kwa msaada wao wa kuendeleza na kukamilisha zoezi hili.

Maoni au mchango wowote wa mawazo unakaribishwa kwa ajili ya uboreshaji wa kitabu hiki kwa matoleo mengine yatakayofuata baadaye.

**Dkt. MBARUSHIMANA Nelson**
**Mkurugenzi Mkuu, REB**

## SHUKRANI

Napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa wale wote walioshiriki kwa hali na mali katika kukiandaa na kukifanikisha kitabu hiki cha mwongozo wa mkufunzi. Kitabu hiki kisingeliwezekana kufanikiwa bila kuwepo wadau mbalimbali walioshiriki; jambo ambalo limenifanya nitoe shukrani zangu za dhati .

Shukrani zangu za kwanza ziwaendee wafanyakazi wa Bodi ya Rwanda ya Elimu ya Msingi walioshiriki katika kuandaa na kuandika kitabu hiki. Napenda kutoa shukrani zaidi kwa wakufunzi wa ngazi zote kwa juhudi zao katika ufanikishaji wa kazi hii ya thamani.

Natoa shukrani kwa uongozi wa shule mbalimbali nchini Rwanda kwa kuwaruhusu walimu kushiriki katika kukiandaa na hata kukikamilisha kitabu hiki.

**Joan MURUNGI**

**Mkuu wa Idara ya Mitaala, Ufundishaji, Ujifunzaji na Zana ( CTLR)**

# YALIYOMO

**VIFUPISHO** ........ iii

**DIBAJI** ........ iv

**SHUKRANI** ........ vi

**SEHEMU I: UTANGULIZI WA JUMLA** ........ 1

1.1. Muundo wa mwongozo wa mkufunzi ........ 1

1.2. Mwelekeo wa ufundishaji ........ 1

1.2.1. Mwelekeo wa kuendeleza uwezo ........ 1

1.2.2. Kuingizwa kwa masuala mtambuka ........ 3

1.2.3. Uangalizi wa wanafunzi wenye mahitaji maalum ........ 4

1.2.4. Mwongozo wa tathmini ........ 5

1.2.5. Mbinu na mikakati ya kuendeleza ufundishaji na ujifunzaji ........ 6

1.2.6. Mbinu za ufundishaji zinazokuza shughuli ya ujifunzaji shirikishi . 6

**SEHEMU 2: SAMPULI YA ANDALIO LA SOMO** ........ 8

**MADA YA 1: MATUMIZI YA KISWAHILI KATIKA MAENEO YA UTAWALA** ... 12

1.1. Uwezo mahususi ........ 12

1.2. Ujuzi wa awali ........ 12

1.3. Masuala mtambuka katika mada ........ 12

1.4. Mwongozo kuhusu kidokezo cha mada ........ 13

1.5. Orodha ya masomo na tathmini ........ 14

**SOMO LA 1: NCHI YETU RWANDA** ........ 15

1.6. Kazi ya utafiti ........ 20

1.7. Muhtasari wa mada ........ 20

1.8. Maelezo ya ziada kwa mkufunzi ........ 20

1.9. Tathmini ya mada ........ 22

1.10. Kazi za ziada ........ 22

1.10.1. Kazi za urekebishaji ........ 22

1.10.2. Kazi jumuishi ........ 23

1.10.3. Kazi za nyongeza ........ 23

**MADA YA 2: KISWAHILI NA FASIHI SIMULIZI ... 24**
2.1. Uwezo mahususi ... 24
2.2. Ujuzi wa awali ... 24
2.3. Masuala mtambuka katika mada ... 24
2.4. Mwongozo kuhusu kazi ya utangulizi wa mada ... 25
2.5. Orodha ya masomo na tathmini ... 26
**SOMO LA 2: DHANA YA FASIHI SIMULIZI ... 27**
**SOMO LA 3: HADITHI ... 32**
2.6. Kazi ya utafiti ... 36
2.7. Muhtasari wa mada ... 36
2.8. Maelezo ya ziada ... 37
2.9. Tathmini ya mada ... 37
2.10. Kazi za ziada ... 38
2.10.1. Kazi za urekebishaji ... 38
2.10.2. Kazi jumuishi ... 38
2.10.3. Kazi za nyongeza ... 38
**MADA YA 3: METHALI NA SEMI FUPIFUPI ... 39**
3.1. Uwezo upatikanao katika mada ... 39
3.2. Ujuzi wa awali ... 39
3.3. Kuingizwa kwa masuala mtambuka katika mada ... 39
3.4. Mwongozo kuhusu kidokezo cha mada ... 40
3.5. Orodha ya masomo na tathmini ... 41
**SOMO LA 4: METHALI NA NAHAU (SEMI FUPI) ... 42**
3.6. Kazi ya utafiti ... 49
3.7. Muhtasari wa mada ... 49
3.8. Maelezo ya ziada kwa mkufunzi ... 49
3.9. Tathmini ya mada ... 49
3.10. Kazi za ziada ... 50
3.10.1. Kazi za urekebishaji ... 50
3.10.2. Kazi jumuishi ... 50
3.10.3. Kazi za nyongeza: ... 51

**MADA YA 4: MJADALA ........................................................................................ 52**

4.1. Uwezo Mahususi upatikanao katika mada ................................................52

4.2. Ujuzi wa awali..........................................................................................52

4.3. Kuingizwa kwa masuala mtambuka katika mada ....................................52

4.4. Mwongozo kuhusu kidokezo cha mada...................................................54

4.5. Orodha ya masomo ...............................................................................54

**SOMO LA 5: MJADALA ........................................................................................ 55**

**SOMO LA 6: MAANDALIZI NA UTEKELEZAJI WA MJADALA......................... 60**

4.6. Kazi ya utafiti ..........................................................................................64

4.7. Muhtasari wa mada..................................................................................64

4.8. Maelezo ya ziada kwa mkufunzi ..............................................................64

4.9. Tathmini ya mada ya nne.........................................................................65

4.10. Kazi za ziada ..........................................................................................67

4.10.1. Kazi za urekebishaji ..........................................................................67

4.10.2. Kazi jumuishi ....................................................................................67

4.10.3. Kazi za nyongeza ..............................................................................67

**MADA YA 5: UTUNGAJI WA INSHA ZA MASIMULIZI ........................................ 68**

5.1. Uwezo upatikanao katika mada...............................................................68

5.2. Ujuzi wa awali..........................................................................................68

5.3. Kuingizwa kwa masuala mtambuka katika mada.....................................68

5.4. Mwongozo kuhusu kazi ya utangulizi wa mada........................................69

5.5. Orodha ya masomo na tathmini ..............................................................69

**SOMO LA 7: UTUNGAJI WA INSHA ZA MASIMULIZI ........................................ 71**

5.6. Kazi ya utafiti ..........................................................................................77

5.7. Muhtasari wa mada..................................................................................77

5.8. Maelezo ya ziada kwa mkufunzi ..............................................................77

5.9. Tathmini ya mada.....................................................................................77

5.10. Kazi za ziada ..........................................................................................78

5.10.1. Kazi za urekebishaji..........................................................................78

5.10.2. Kazi jumuishi ....................................................................................79

5.10.3. Kazi za nyongeza: .............................................................................80

**Marejeo ........................................................................................................ 81**

# SEHEMU I: UTANGULIZI WA JUMLA

## 1.1. Muundo wa mwongozo wa mkufunzi

Kitabu hiki ni mwongozo wa mkufunzi katika mchakato wa ufundishaji wa somo la Kiswahili, mwaka wa pili, michepuo mingine katika vyuo vya ualimu nchini Rwanda. Kimetayarishwa kwa mwelekeo wa mtaala uegemeao katika uwezo. Mwongozo wa mkufunzi huu unaundwa na sehemu tatu.

Sehemu ya kwanza inahusu utangulizi wa jumla ambao unajishughulisha na namna ya kufundisha na kujifunza Kiswahili, kukuza uwezo wa wanafunzi katika ufundishaji na ujifunzaji, jinsi ya kushughulikia masuala mtambuka na inatoa mwongozo kuhusu tathmini.

Sehemu ya pili ni sampuli ya andalio la somo ambayo inaonyesha vipengele vya somo na jinsi ya kuandaa somo hilo.

Sehemu ya tatu inahusu uendelezaji wa mada tofauti. Sehemu hii inatoa taarifa kuhusu uwezo upatikanao katika mada, ujuzi wa awali wa wanafunzi kuhusu mada inayofundishwa, mwongozo kuhusu vidokezo, orodha ya masomo, mwongozo kuhusu namna ya kufanikisha masomo mbalimbali, maelezo ya ziada, tathmini ya mada, kazi za ziada ambazo zinajumuisha: kazi za urekebishaji, kazi jumuishi na kazi za nyongeza.

Majibu ya kazi zote, tathmini ya mada na kazi za nyongeza zilizomo katika kitabu cha mwanafunzi-mkufunzi yanapatikana katika sehemu hii.

## 1.2. Mwelekeo wa ufundishaji

### 1.2. 1. Mwelekeo wa kuendeleza uwezo

Kwa kusitawisha mafanikio ya elimu, Serikali ya Rwanda ilianzisha mtaala uegemeao katika uwezo katika shule za elimu ya jumla (CBC). Aina hii ya mtaala ilizinduliwa mwezi wa Aprili 2015 na kutekelezwa kuanzia mwaka wa 2016. Mtaala huu ulibuniwa ili kukidhi mahitaji ya wanafunzi, jamii na soko la ajira.

Pamoja na mbinu ya ujifunzaji wa jumla inayomchukua mwanafunzi kama kiini cha ufundishaji, mtaala huu unalazimisha mabadiliko makubwa katika mbinu za ufundishaji na matumizi ya mbinu nyingi za tathmini kwa kuzingatia tathmini endelezi.

Hii ina maana kubwa kwa mkufunzi na utoaji wa msaada na mwongozo kwa shule ili kuhakikisha utekelezaji bora wake.

Mwalimu ana wajibu mkubwa katika kuboresha elimu na ndiye jambo la msingi katika kuamua mafanikio ya wanafunzi wa shule za chekechea na shule za msingi.

Ndiyo maana ni muhimu kuwapa wanafunzi uwezo ambao utawawezesha kutekeleza kwa ufanisi mtaala uegemeao katika uwezo kama inavyotarajiwa.

**Jinsi ya kuendeleza uwezo**

Uwezo hupatikana kwa muda mrefu kupitia mkusanyiko wa athari zitokanazo na mbinu za ujifunzaji unaotilia maanani uwezo. Ikumbukwe kwamba uwezo wa mwanafunzi hauendelezwi katika ombwe bali umeunganishwa wakati huo huo.

Kuhusisha wanafunzi katika ujifunzaji ni muhimu kwa mafanikio ya mtaala uegemeao uwezo.

Mwanafunzi anahitaji kuingizwa katika hali za kujifunza zilizo tofauti na katika hali ya vitendo ambapo ujifunzaji unaendelea mara kwa mara.

Kupitia mbinu shirikishi, wanafunzi wanapashwa kufikiria sana, kufanya utafiti, kutatua matatizo, kuwa wabunifu na wagunduzi, kuwasiliana na kushirikiana.

Miongoni mwa mbinu shirikishi, kuna hizi zifuatazo: maigizo, kazi za makundi, maswali na majibu, mbinu za ziara, kazi mradi,tukio,bungua bongo, majadiliano, kazi ya utafiti, michezo na mbinu nyingine nyingi.

Mfano unaofuata unaonyesha namna ambavyo wakufunzi wanaweza kusaidia wanafunzi kuendeleza uwezo wao.

**Mfano:**

a) Mkufunzi aweke wanafunzi katika makundi na kuwapatia zoezi linalowasaidia kuendeleza uwezo wao katika mada fulani inayofundishwa katika Lugha ya Kiswahili.

   **Kwa mfano**: Jadili umuhimu wa kutunza mazingira ya shuleni kwa wanafunzi.

b) Kundi limchague kiongozi na katibu wa kuandika maoni yanayotolewa katika majadiliano.

c) Baada ya muda uliokuwa umetolewa kumalizika, majadiliano yasimamishwe na katibu kutoka makundi tofauti awasilishe matokeo yao.

d) Uwezo unaoendelezwa ni: Ushirikiano, mawasiliano, tafakuri tunduizi, uongozi na usimamizi, utafiti na usuluhishaji wa matatizo, na ujifunzaji wa kudumu.

Zaidi ya uwezo upatikanao katika masomo mahususi, wanafunzi wanaendeleza pia uwezo wa kijumla unaopatikana kupitia hali mbali mbali.

### 1.2.2. Kuingizwa kwa masuala mtambuka

Katika kitabu hiki, imetolewa mifano ya jinsi ya kushughulikia masuala mtambuka katika somo la Kiswahili, na mkufunzi awaongoze wanafunzi katika ujifunzaji na kutumia masuala mtambuka yafuatayo:

a) **Elimu jumuishi:** Katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji, mkufunzi analazimishwa kubainisha wanafunzi walimu wenye mahitaji maalumu na kuwaandalia mazoezi kufuatana na mahitaji yao. Shirikisha wanafunzi walimu wote katika kazi walizoandaliwa bila upendeleo.

   **Mfano:** Mpatie mwanafunzi aliye na ulemavu wa mwili (asiyeona) jukumu la kuongoza mjadala.

   Mtafutie mahali pa kukaa na vifaa vya kutumia kufuatana na mahitaji yake.

b) **Usawa wa kijinsia:** Katika mchakato wa ufundishaji, mkufunzi analazimishwa kuandaa mazoezi ambayo yanashirikisha wavulana na wasichana na kuwasaidia kutumia uwezo wao ipasavyo.

   Hakuna kazi ambayo inatarajiwa kuwa ya msichana au mvulana. Wakufunzi wangehakikisha kwamba wasichana na wavulana wanachukua nafasi sawa wakishiriki katika kazi za makundi, mijadala na midahalo.

c) **Elimu kuhusu amani na maadili:** Katika mchakato wa ufundishaji, mkufunzi analazimishwa kuwahimiza wanafunzi kuwa na uvumilivu, ushirikiano, kuwa na moyo wa kufanya kazi kwa pamoja, kusaidiana kwa pande zote, kuheshimu maoni ya wengine, kuheshimu maagizo na kuwepo kwa mazingira mazuri ya kujifunzia.

d) **Mafunzo kuhusu desturi ya usanifishaji:** Katika mchakato wa ufundishaji, wanafunzi wanalazimishwa kutunza vizuri vifaa vya shuleni na kutoviharibu kama vile vitabu, madaftari, madawati, n.k. Mkufunzi pia anaweza kuwasaidia kuchagua vitabu vya kusoma vinavyohusiana na masomo yao lakini vinavyokubaliwa katika mfumo wa elimu ya Rwanda.

e) **Mazingira na maendeleo endelevu:** Katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji masuala ya mazingira na maendeleo endelevu yatashughulikiwa kama ifuatavyo:

   - Mkufunzi aeleze wanafunzi umuhimu wa mazingira safi iwe nyumbani, shuleni, hospitalini, n.k.
   - Wanafunzi wasichafue madarasa kwa kutupa karatasi au uchafu wowote katika mazingira ya shule wakati wa kusoma na baada ya maosomo. Washauriwe kutotema mate au kupenga ovyo mahali popote.
   - Mkufunzi aweke maagizo ya kufanya usafi darasani na katika busitani za shule.

f) **Mafunzo kuhusu uzalishajimali/ujasiriamali:** Katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji mafunzo kuhusu uzalishajimali/ujasiriamali yatashughulikiwa wakati ambapo: Wanafunzi wanao uwezo wa kutunga mashairi, hadithi na michezo ya kuigiza wakashiriki katika mashindano tofauti na kupewa zawadi au wakaunda klabu za michezo ya kuigiza na ambapo wanawaalika watu kutazama michezo ya kuigiza na kulipa pesa za kuingia. Hii inawasaidia wanafunzi kufahamu kuwa Kiswahili kinaweza kuwa chanzo cha shughuli za uzalishaji mapato na kujipatia ajira.

g) **Elimu kuhusu ufahamu wa ujinsia:** Katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji, mkufunzi atoe maagizo na kazi zisizochochea unyanyasaji wa kijinsia. Pia, anaweza kutoa kazi au vifungu vya habari vinavyoshughulikia afya ya uzazi na mpango wa kuboresha uzazi.

h) **Mafunzo kuhusu mauaji ya kimbari:** Katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji, mkufunzi atoe kazi na mada za kuzungumzia au kujadili madhara ya mauaji ya kimbali kwa jamii na jinsi ya kutupilia mbali itikadi yake.

Mkufunzi awasaidie wanafunzi kuingiza masuala mtambuka haya kwa kila somo wanalojifunza na kutafuta suluhisho kuhusu masuala hayo.

### 1.2.3. Uangalizi wa wanafunzi wenye mahitaji maalum

Malengo ya ujifunzaji na ufundishaji humhusu kila mwanafunzi darasani bila ubaguzi au utengano wowote. Kwa hiyo, inambidi mkufunzi kuyakumbuka na kuyahudumia makundi mbalimbali ya wanafunzi wenye mahitaji maalumu au ya kipekee katika ujifunzaji wao. Hao ni kama vile wanafunzi wenye tatizo la kutoona, kutosikia, kutoandika, kutosoma, kutozungumza na matatizo mengine ya kiakili.

Kuna watu wanaofikiri kwamba ni kazi ngumu kushughulikia wanafunzi wenye mahitaji tofauti. Lakini, kwa kushirikiana shuleni, kwa kushirikiana na familia ya wanafunzi hao na jamii kwa ujumla, na kubadilisha mbinu za ufundishaji utakidhi mahitaji ya wanafunzi wote wakiwemo na wale wenye mahitaji maalum kwani baadhi yao huelewa masomo haraka haraka na wengine kidogokidogo.

Mwanafunzi angeweza kujitayarisha kushughulikia mahitaji maalumu ya kielimu kwa kuiga vitendo bora vya wakufunzi wao.

Kwa kuwashirikisha wote, mkufunzi hulazimishwa:

- Kutayarisha mazoezi ya aina aina kulingana na mahitaji ya kila mwanafunzi.
- Kukumbuka kwamba wanafunzi hujifunza kwa njia tofautitofauti. Kwa hiyo, mkufunzi anapaswa kutoa kazi mbalimbali za ujifunzaji kama vile (umithilishaji, muziki na uimbaji, kazi za nje ya darasa na michezo mbalimbali).

- Kushikilia usalama wa darasa na kuondoa usumbufu wowote. Hii itawasaida wanafunzi wenye mahitaji maalumu kutopotoshwa na mazingira na hivyo watafuata mkufunzi vizuri.
- Kulirahisisha somo kwa kiasi kwamba kila mwanafunzi hulielewa. Wanafunzi wenye mahitaji maalum huwa na vikwazo kuelewa wanapopewa maagizo mengi kwa mfululizo. Bora kutumia sentensi rahisi na zinazoeleweka haraka ili kumsaidia kuelewa kilichoulizwa.
- Kutumia sentensi sahili zinazoeleweka unapoeleza maana au dhana mpya au unapotoa maagizo.
- Kutumia viungo vya mwili na ishara unapofundisha.
- Kuweka mwanafunzi aliye na mahitaji maalumu katika jozi lenye wanafunzi wengine ambao hawana mahitaji yao ya kipekee. Waache wafanye kazi pamoja ili mmoja ajifunze kutoka kwa mwenzake. Hakikisha kwamba wote wanashiriki kufanya kazi iliyotolewa. Wanafunzi wote watanufaika na mbinu hii.
- Kufanya kazi kuwa hai kwani inajulikana kwamba wanafunzi hujifunza kupitia mbinu mbalimbali. Wanafunzi wenye mahitaji maalum huenda wasifaulu katika mbinu moja na kufaulu katika mbinu nyingine. Kwa mfano, tumia picha na sauti kulingana na hali iliyopo.
- Kutumia vifaa halisi anavyoweza kuhisi na kugusa kwa yule aliye na matatizo ya kutoona,
- Kurahisisha kazi katika hatua ndogondogo au malengo ya ujifunzaji. Anzia kwenye kazi rahisi kabla ya kufikia ile ngumu.
- Kusaidia mwanafunzi kidogo kidogo na kumwacha kufanya kazi huku akishirikiana na wengine katika kazi za makundi.

### 1.2.4. Mwongozo wa tathmini

Tathmini ni jambo muhimu sana katika njia hii ya ufundishaji na ujifunzaji. Lengo kuu la tathmini ni kupima maendeleo ya somo ambapo mkufunzi huweza kuchagua aina ya tathmni kulingana na malengo yake.

- **Tathmini endelezi**

  Tathmini hii hulenga kupima jinsi ufundishaji na ujifunzaji unavyoendelea au kama makusudi au malengo ya ufundishaji na ujifunzaji yamefikiwa kwa kiwango fulani ili kuamua kuhusu uboreshaji wa baadaye. Tathmni hii inafanywa wakati masomo yangali yanaendelea na hulenga kuangalia uhusiano uliopo kati ya ufundishaji na ujifunzaji yaani uhusiano kati ya mkufunzi na mwanafunzi. Hujumuisha upimaji wa mwenendo wa somo kabla somo lifikie kikomo. Tathmini endelezi inapaswa kuwa na dhima mwafaka katika ufundishaji na ujifunzaji. Inambidi mkufunzi kuwahamasisha wanafunzi kufanya mazoezi na majaribio binafsi, mazoezi ya makundi, kwa kutumia mbinu zinazoegemea kwenye uwezo, maadili na mwenendo mwema kulingana na kila somo husika.

- **Tathmini ya jumla**

Kila tathmini huwa na dhima yake katika ufundishaji na ujifunzaji. Kwa mfano, tathmini ya mwishoni mwa mada itafikiriwa na itafanyika mwishoni mwa mada nzima kabla ya kutangulia mada nyingine. Aidha, tathmini inayofanyika mwishoni mwa muhula na mwishoni mwa mwaka zitakuwa mojawapo ya tathmini za jumla na wakati huu hulenga kurekodi ujuzi, uwezo, maadili na mwenendo mwema miongoni mwa wanafunzi kiasi kwamba wakufunzi, viongozi wa shule na wazazi hupata na kuchunguza matokeo ya tathmini iliyofanywa. Tathmni zilizopendekezwa katika kitabu cha mwanafunzi zitamwelekeza mkufunzi kubashiri matatizo yaliyopo kwa ajili ya kuboresha ufundishaji na ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili kwa kiwango cha kuwaelekeza wanafunzi kupata uwezo walio nao katika somo hili. Hivyo basi, tathmini zilizopendekezwa katika kitabu cha mwanafunzi ni msingi wa mambo mengine ambayo mwanafunzi atayakuta katika miaka mingine ya masomo yake ya Kiswahili kwa shule za sekondari.

### 1.2.5. Mbinu na mikakati ya kuendeleza ufundishaji na ujifunzaji

Katika kuendeleza ufundishaji na ujifunzaji, mkufunzi achunguze mambo yafuatayo:

- Upekee wa somo,
- Kielelezo cha somo,
- Malengo maalum ya kutimiza,
- Kuchunguza idadi ya vipindi mahususi kwa madhumuni ya kutimiza malengo ya somo,
- Maelekezo muhimu kuhusu vifaa vya ufundishaji na ujifunzaji vinavyopatikana katika mazingira halisi,
- Jinsi wanafunzi watakavyokaa darasani,
- Vifaa vya wanafunzi wenye mahitaji maalum ya kielimu,
- Uwezo na mtindo wa ujifunzaji.

### 1.2.6. Mbinu za ufundishaji zinazokuza shughuli ya ujifunzaji shirikishi

Ili kufanikisha malengo ya somo lake, mkufunzi azingatie njia zifuatazo:

- **Njia Shirikishi**: Njia shirikishi hutumia makundi ya wanafunzi ambapo mkufunzi huwawezesha wanafunzi kushiriki katika kitendo cha ufundishaji na ujifunzaji. Kinachopaswa kufanywa hapa ni kuwapatia wanafunzi wote fursa ya kushiriki katika shughuli zinazopendekezwa katika kitabu cha mwanafunzi. Hali hii hutokana na mazingira yanayojengwa na mkufunzi ambapo kila mwanafunzi ndiye ambaye huchukuliwa kama kiini cha ufundishaji na ujifunzaji. Hivyo basi, wanafunzi watatumia

makundi yao kwa kufanya shughuli zote watakazoombwa na mkufunzi kama vile majadiliano, midahalo na mazungumzo ya aina tofauti kama yalivyopendekezwa katika kitabu cha mwanafunzi.

- **Njia ya kibinafsi:** Njia hii inahusu kazi binafsi za kila mwanafunzi ambapo atapewa kazi ama mazoezi yake binafsi iliaweze kufikia kiwango cha umilisi wa lugha kinachotarajiwa. Baada ya kufanya kazi na mazoezi hayo, ni vyema mkufunzi akumbuke kuambatanisha njia aliyoitumia na njia shirikishi kwa kumwomba mwanafunzi achunguze maoni na hoja za wanafunzi wenzake katika makundi yao. Katika njia ya kibinafsi, mkufunzi anaweza kuomba mwanafunzi, kwa mfano, kujisomea kifungu cha habari, kutambua maana za maneno mapya na kuyatumia katika sentensi zake, n.k.
- **Maswali na majibu**: Mara nyingi somo huchukua mwelekeo wa majadiliano kati ya mkufunzi na wanafunzi. Kuhusiana na mbinu hii, mwalimu atawauliza wanafunzi maswali mbalimbali nao watajibu maswali hayo. Kwa upande mwingine, wanafunzi wanaweza kumwuliza mkufunzi wao naye akawajibu. Vilevile, maswali na majibu haya yanaweza kujitokeza kati ya wanafunzi wenyewe. Katika hali hii, mkufunzi atawaelekeza wanafunzi wake kujitafutia majibu kwa maswali wanayouliza huku akiwapa maelekezo muhimu au mwongozo unaofaa kwa kusahihisha makosa wanayoyafanya.
- **Maelezo ya mkufunzi**: Mwanafunzi hupewa muda wa kushiriki yeye binafsi katika somo. Katika njia hii, mkufunzi atakuwa mwelekezi na shughuli yake muhimu itaegemea kuwaongoza wanafunzi kupata ufahamu na uelewa unaofaa. Kwa hiyo, mkufunzi atatumia mbinu hii kwa kueleza mambo yatakayohitaji maelezo yake ili kufanikisha somo lake.

## SEHEMU 2: SAMPULI YA ANDALIO LA SOMO

**Jina la shule: ..................................Jina la Mkufunzi: ..................................**

| **Muhula** | **Tarehe** | **Somo** | **Mwaka** | **Mada** | **Idadi ya masomo** | **Muda** | **Idadi ya wanafunzi** |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **1** | 28/1/2020 | Kiswahili | 2 | 1 | Masomo 1 | Dakika 40 | 50 |
| **Aina ya wanafunzi wenye mahitaji maalum ya kielimu watakaoshughulikiwa katika somo, idadi yao kulingana na mahitaji yao** | | | | 2: Wenye ulemavu wa viungo vya mwili | | | |

| | |
|---|---|
| **Mada** | **Matumizi ya kiswahili katika maeneo ya utawala** |
| **Uwezo unaopatikana katika mada** | Kuzungumza na kuandika kwa ufasaha matini fupifupi kwa kutumia msamiati unaofaa katika mazingira ya utawala. |
| **Somo lenyewe** | Kusoma kifungu: Nchi yetu Rwanda |
| **Malengo ya kujifunza** | Baada ya kusoma na kufahamu kifungu, mwanafunzi atakuwa na uwezo wa:<br>- Kutaja ngazi za utawala na viongozi wakuu wa serikali.<br>- Kuonyesha msamiati unaofaa katika maeneo ya utawala.<br>- Kutumia msamiati katika sentensi.<br>- Kuorodhesha sikukuu za kitaifa.<br>- Kutaja aina mbalimbali za vitambulisho vinavyotumiwa. |
| **Mahali somo litakapofundishiwa** | Darasani |
| **Vifaa au zana kwa wanafunzi wote** | Kitabu cha mwanafunzi, kitabu cha mkufunzi, ubao, chaki, madaftari, kalamu. |
| **Vitabu vya rejea** | Kitabu cha mwanafunzi mwaka wa pili, Mwongozo wa mkufunzi, Kamusi ya Kiswahili Sanifu. |

| Muda na hatua | Mbinu za kufundishia na kujifunzia<br>**Kazi katika makundi:** Mara nyingi wanafunzi watafanyia kazi yao katika makundi kwa kushirikiana ili wafanikiwe na mambo kadhaa.<br>**Kazi ya kibinafsi:** Wanafunzi watapata muda mfupi wa kufanya kazi ya kipekee. | | Uwezo wa jumla na masuala mtambuka vielezewe + maelezo mafupi |
|---|---|---|---|
| | **Wajibu wa mkufunzi** | **Wajibu wa mwanafunzi** | |
| **Utangulizi**<br>**Dakika 5** | - Mkufunzi awaamkie wanafunzi.<br>- Mkufunzi awaulize wanafunzi maswali ya kuwachangamua na maswali mengine kuhusu mchoro unaotangulia mada. Mkufunzi akiuliza maswali, achague wanafunzi wa kujibu kwa kuchanganya wavulana na wasichana. | - Wanafunzi waiitikie maamkizi ya mkufunzi.<br>- Wanafunzi watajibu maswali yote yaliyoulizwa na mkufunzi. | **Uwezo wa jumla:** Ushirikiano, utawala binafsi na stadi za maisha pamoja na mawasiliano katika lugha rasmi. |
| **Somo lenyewe**<br>Dakika 25 | - Mkufunzi aunde makundi ya wanafunzi tisa tisa ya wavulana kwa wasichana. Baadaye, awape vitabu vya wanafunzi na awaombe kusoma kwa sauti ndogo kifungu "Nchi yetu Rwanda".<br>- Mkufunzi awaombe wanafunzi kusoma tena kifungu cha habari na kujibu maswali ya ufahamu. | - Wanafunzi wakae katika makundi ya wanafunzi tisa tisa na kusoma kifungu walichopewa kwa kutumia muda maalum.<br>- Wanafunzi wasome tena kifungu cha habari na kujibu maswali ya ufahamu. | **Uwezo wa jumla:** Tafakuri tunduizi,<br>Ushirikiano, utawala binafsi na stadi za maisha.<br>Mawasiliano katika lugha rasmi.<br>**Utafiti:** Kwa kujibu maswali ndani ya makundi, wanafunzi watafanya utafiti, watashirikiana kupata majibu, na kuchagua |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | - Mkufunzi awaombe wanafunzi kutafuta maneno magumu katika kifungu cha habari na kutumia Kamusi ya Kiswahili Sanifu wanapoyafafanua.<br><br>- Mkufunzi awaombe wanafunzi kumwambia maneno ambayo wameshindwa kuyafafanua.<br><br>- Mkufunzi awape wanafunzi mwongozo wa kusoma kifungu cha habari.<br><br>- Mkufunzi awape wanafunzi muda wa kusoma kwa sauti kubwa hivi akiwasahihisha.<br><br>- Mkufunzi awaombe wanafunzi kujichagulia wasimamizi wa kuandika majibu ya maswali ya ufahamu kwenye ubao kundi kwa kundi. Mkufunzi awaongoze wanafunzi ili majibu yanayofanana yasiandikwe mara mbili kwa kutumia muda vizuri. Mkufunzi asahihishe majibu ya wanafunzi itakiwavyo. | - Wanafunzi watafute maneno magumu na kuyaandika mahali fulani, kisha wayafafanue kwa kutumia Kamusi ya Kiswahili Sanifu.<br><br>- Wanafunzi wamwambie mkufunzi maneno yanayowashinda na kujaribu kuyafafanua wakisaidiwa na mkufunzi.<br>- Wanafunzi wasikilize kwa makini namna mkufunzi anavyosoma na waige mwenendo na lafudhi nzuri.<br>- Wanafunzi wasome mmoja baada ya mwingine kwa kubadilisha makundi.<br><br>- Wanafunzi waandike matokeo ya makundi yao yenye kujibu maswali ya ufahamu wa kifungu cha habari kundi baada ya kundi jingine, mvulana na msichana kimpango. Wamfuate mkufunzi iwapo kuna majibu ambayo yanahitaji masahihisho yake. | viongozi wa makundi hivi wakiwasiliana katika lugha rasmi.<br><br>**Masuala mtambuka:**<br>- **Usawa wa kijinsia:** Wanafunzi wafanye kazi pamoja; wasichana na wavulana na wapewe fursa sawa.<br><br>- **Mafunzo kuhusu amani na maadili:** Kwa kufanyia kazi katika makundi, wanafunzi wajadiliane hivi wakitoa na kupokea fikra tofauti kwa amani.<br>- **Elimu jumuishi:** Kila mwanafunzi atapewa fursa ya kushiriki katika somo. |

| | | | |
|---|---|---|---|
| **Hitimisho**<br>Dakika 10 | - Mkufunzi awaombe wanafunzi kufanya muhtasari wa somo.<br><br>- Mkufunzi awape wanafunzi swali moja la tathmini.<br><br>- Mkufunzi awaombe wanafunzi kusahihisha maswali. | - Wanafunzi wafanye muhtasari wa somo.<br><br>- Wanafunzi wajibu swali hilo kwenye karatasi na kumpa mkufunzi karatasi hizo ili azisahihishe.<br><br>- Wanafunzi wasahihishe maswali waliyopewa. | **Uwezo wa jumla:**<br>**Tafakuri tunduizi na stadi ya utatuzi wa matatizo:** wanafunzi wafikirie kwa upana na kujibu maswali wenyewe. |
| **Tathmini ya mkufunzi** | | | |

# MADA YA 1

# MATUMIZI YA KISWAHILI KATIKA MAENEO YA UTAWALA

## 1.1. Uwezo mahususi

Kuzungumza na kuandika kwa ufasaha matini fupifupi kwa kutumia msamiati unaofaa katika mazingira ya utawala.

## 1.2. Ujuzi wa awali

Katika mwaka wa kwanza na katika vidato vya chini, wanafunzi hawa walikuwa na mada tofauti za msamiati katika mazingira tofauti. Mada hizi ziliwajengea uwezo wa: kujadili na kutumia msamiati kimazungumzo na kimaandishi.

## 1.3. Masuala mtambuka katika mada

Katika masomo ya mada hii kwenye vifungu, michoro au picha, utumiaji wa msamiati katika sentensi, sarufi, matumizi ya lugha, kusikiliza na kuzungumza, kuandika, na katika mazoezi au kazi mbalimbali; mkufunzi awaongoze wanafunzi katika ujifunzaji na kutumia masuala mtambuka yafuatayo:

- **Elimu kuhusu amani na maadili**
    - Katika majadiliano, wanafunzi hutarajiwa kutokasirika ovyo na kusikiliza wengine wakitoa hoja zao. Majadiliano haya huwafundisha wahusika kusikilizana na kuelewana kama njia mojawapo ya kujenga amani imara na kuchukua uamuzi mmoja. Kwa hiyo, wanafunzi watapata mwanya wa kufikiria suala hili.
    - Kwa kutunga sentensi, mkufunzi awaongoze kutunga sentensi zenye mafunzo yanayohusu amani na maadili.
- **Mafunzo kuhusu desturi ya usanifishaji**
  Kwa kufanya kazi yoyote, ama kuandika inafaa kuchunguza kama unafuata taratibu za kuandika.
- **Elimu Jumuishi**
  Makundi ya wanafunzi wenye mahitaji maalumu ya kielimu kama vile: wanafunzi wenye matatizo ya ulemavu, wanafunzi wenye kipaji maalumu katika uwezo wa kujifunza, na kadhalika lazima washughulikiwe vilivyo.

Kumbuka kuwa wanafunzi wenye matatizo kama haya ni kama wengine; walikuja shuleni ili wapate maarifa na maadili yanayotakiwa. Kwa hiyo, ni lazima wewe mkufunzi uwasaidie ipasavyo.

- **Mazingira na maendeleo endelevu**

  Mkufunzi, kupitia kazi za msamiati na sarufi, anaweza kueleza umuhimu wa kuhifadhi mazingira kwa maisha ya watu.

- **Usawa wa Jinsia**
  - Mkufunzi katika mifano yote, ni lazima kutoa mifano inayoonyesha usawa wa jinsia;
  - Katika mazoezi ya kutunga sentensi, ni vizuri kutunga sentensi ambazo zinaeleza na kutoa maelezo kuhusu usawa wa jinsia;
  - Kazi katika makundi, ni vizuri kupanga wasichana na wavulana katika kundi moja ili darasani pasiwe na kundi la jinsia moja.

- **Elimu kuhusu uzalishajimali/ujasiriamali**

  Kazi na mazoezi tofauti yanayotayarishwa darasani yatakuwa yanahusisha suala mtambuka hili. Wanafunzi watapewa fursa ya kufikiria na kuzungumzia kuhusu suala hili kwa sababu masomo yote wanayoyasoma ni ya kuwazindua ili wajitegemee nyakati zijazo.

- **Mafunzo kuhusu mauaji ya kimbari**

  Katika maelezo yake hasa kwenye sikukuu na siku maalum katika mada hii wanafunzi pamoja na mkufunzi wao watazumgumzia kuhusu suala mtambuka hili.

## 1.4. Mwongozo kuhusu kidokezo cha mada

- Kwa kutangulia mada, mkufunzi aulize maswali ambayo yatawasaidia wanafunzi kufunua mada hii.
- Wanafunzi wanaweza kushindwa kutoa majibu sahihi mwanzoni, lakini wanaweza kufanikiwa kwa kupitia masomo tofauti, mazoezi, vifungu, na kazi nyingine zilizotayarishwa kwenye mada hii.

## 1.5. Orodha ya masomo na tathmini

| Kichwa cha somo | Malengo ya kujifunza | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|
| **1. Nchi yetu Rwanda** | **Maarifa na ufahamu:** Kufafanua msamiati kuhusu maeneo ya utawala.<br>**Stadi**: Kutumia msamiati unaohusu maeneo ya utawala katika sentensi na matini.<br>**Maadili na mwenendo mwema:** Kuonyesha moyo wa heshima wakati wa majadiliano na maongezi. | **6** |
| **Tathmini ya mada** | | **1** |
| **Vipindi vyote vya mada ya 1** | | **7** |

# SOMO LA 1: NCHI YETU RWANDA

**a) Malengo ya ujifunzaji**

Baada ya kufundisha somo hili, mwanafunzi atakuwa na uwezo wa:

- Kutaja ngazi za utawala na viongozi wakuu wa serikali,
- Kuonyesha msamiati unaofaa katika maeneo ya utawala,
- Kuorodhesha sikukuu za kitaifa,
- Kutaja aina mbalimbali za vitambulisho vinavyotumiwa,
- Kutunga sentensi kwa kutumia majina ya viongozi na ngazi za utawala,
- Kuchora kielelezo cha ngazi ya utawala nchini Rwanda,
- Kutunga matini fupi akitumia majina ya viongozi na aina mbalimbali za vitambulisho,
- Kuheshimu viongozi na watu wengine wanaopatikana katika maeneo ya utawala,
- Kueleza matumizi ya ngeli ya PA-M-KU.

**b) Zana za ufundishaji**

Ili somo hili liweze kufika kwenye malengo yake, ni lazima mkufunzi ajaribu kutafuta zana za ufundishaji zitakazomsaidia kufanikisha somo lake na kukidhi mahitaji ya wanafunzi na malengo ya somo husika. Katika somo hili zana muhimu ni:

- Kitabu cha mwanafunzi,
- Mwongozo wa mkufunzi,
- Picha,
- Ramani ya Rwanda,
- Michoro mbalimbali,
- Ubao,
- Chaki na vifaa vinavyoweza kuwasaidia wanafunzi kuelewa somo akitilia mkazo kuhusu hali za wanafunzi wanaohitaji uangalifu maalum kama wanafunzi wenye ulemavu mbalimbali.

Vifaa hivi vitaandaliwa kulingana na mazingira ya shule. Kwa hiyo, mkufunzi anaweza kuandaa vifaa kadhaa vinavyoweza kumsaidia kufanikisha somo lake. Ikiwezekana, hakikisha kuwa kuna vifaa kwa wanafunzi wenye mahitaji maalumu. Unapowapa wanafunzi kazi mbalimbali, hakikisha kuwa wanafunzi wenye mahitaji maalumu wamepewa kazi tofauti zitakazowawezesha kupata

ujuzi uliokusudiwa. Baadhi ya wanafunzi wenye matatizo ya kiakili huenda wasiweze kuchora lakini wakawa na uwezo wa kutumia rangi mbalimbali chini ya usaidizi wako au wenzao. Mkufunzi anapaswa kuwa mbunifu ndiyo sababu yeye mwenyewe lazima ajibunie vifaa visaidizi mbalimbali.

**c) Ujuzi wa awali/Marudio/Utangulizi**

Somo hili linajishughulisha na matumizi ya lugha ya Kiswahili katika mazingira maalum yaani utawala. Mkufunzi aanze somo kwa kuwaamkia wanafunzi. Wanafunzi watajibu maamkizi ya mkufunzi kisha atangulize somo kwa kuwauliza maswali mepesi ya kuwachangamsha. Maswali haya yanapaswa kuwa na uhusiano na somo jipya.

Mkufunzi atakachokifanya ni kuwashirikisha wanafunzi wake ili waweze kuwasiliana kuhusu msamiati wa kiutawala, kisha atafanya chochote ili awawezeshe wanafunzi kufika kwenye kile anachotaka kufundisha.

**d) Maelekezo kuhusu kazi za ujifunzaji**

Kwenye hatua hii, mkufunzi atafute mbinu mbalimbali zitakazomwezesha kufika kwenye malengo ya somo lake. Katika somo hili, mkufunzi atatilia mkazo kwenye:

- **Utumiaji wa makundi ya wanafunzi**: Kwa sababu mwanafunzi ndiye kiini cha ufundishaji na ujifunzaji ni lazima mbinu hii itumiwe ili kumshirikisha mwanafunzi katika mambo yote yanayofanyiwa darasani. Wanafunzi watatumia makundi yao kwa kufanya kazi zote watakazopewa na mkufunzi na zile zipatikanazo katika kitabu cha wanafunzi.
- **Fikiri-Jozi-Changia:** Mbinu hii itatumiwa mahali ambapo kazi inaomba kufanyika kwa jozi.
- **Kazi binafsi kwa wanafunzi**: Itakuwa lazima kila mwanafunzi apewe kazi/mazoezi yake binafsi (kwa mfano: kusoma kifungu cha habari, kufanya majaribio, mitihani mbalimbali na hata kazi za nyumbani).
- **Maswali na majibu**: Mara nyingi somo huwa na majadiliano kati ya mkufunzi na wanafunzi. Kuhusiana na mbinu hii, mkufunzi atawauliza wanafunzi maswali mbalimbali nao watajibu maswali hayo. Vilevile, wanafunzi kwa upande wao wanaweza kumwuliza mkufunzi maswali kadhaa naye akawajibu. Tena, maswali na majibu haya yanaweza kuwa kati ya wanafunzi wenyewe.
- **Maelezo ya mkufunzi**: Mbali na kuwa mwanafunzi hupewa kipaumbele katika somo, mkufunzi angali msuluhifu katika somo lake. Kwa hiyo, mkufunzi atatumia mbinu hii kwa kueleza mambo yatakayohitaji maelezo yake ili kufanikisha somo lake.

**e) Majibu:** Yafuatayo ni majibu ya kazi zilizotayarishwa katika somo hili:

**Kidokezo:** ***Haya ni maswali ya kumwingiza mwanafunzi katika somo hili kwa urahisi. Ni maswali yanayoamsha upekuzi au udadisi kwa wanafunzi. Hali kadhalika, hii ni kazi itakayomsaidia mkufunzi kutangulia somo kwa urahisi. Wanafunzi wapewe muda wa kusoma maswali hayo.Majibu yaliyopendekezwa kuhusu kidokezo ni haya yufuatayo:***

Hii ni ramani ya Rwanda. Inaonyesha majimbo na wilaya zake

**Kusoma na ufahamu: Nchi yetu Rwanda**

**Kazi ya 1 :** ***Mkufunzi aweke wanafunzi katika makundi madogo madogo kisha awaombe kuchunguza na kueleza shughuli zinazoendelea kwenye mchoro.***

**Jibu:** Kuna kiongozi anayehutubia watu wanaokaa mbele yake wakiwa na vifaa tofauti k.v. majembe, beleshi na reki. Kuna pia ofisi ya Kata na bendera. Huenda kiongozi huyu akawa Katibu Mtendaji wa Kata anayehutubia wananchi wa Kata baada ya kazi ya Umuganda. Watu hawa wanasikiliza mawaidha ya kiongozi wao.

**Kazi ya 2:** ***"Kusoma na kufahamu" ni mojawapo ya stadi zinazotarajiwa kwa mwanafunzi wa lugha. Usomaji mzuri wa kifungu husaidia kukifahamu, na ndiyo sababu mkufunzi anapaswa kuwasaidia wanafunzi wanaposoma kifungu, kwa kuzingatia matamshi bora ya maneno, hasa maneno mapya, matumizi ya alama za uakifishaji, n.k.***

***"Nchi yetu Rwanda" ni kifungu. Inapendekezwa kisomewe katika makundi ya wanafunzi wanne. Mkufunzi awe makini ili asahihishe makosa ya kusoma yanayoweza kujitokeza. Yafuatayo ni majibu:***

1) Nchi ya Rwanda inapatikana kwenye bara la Afrika.
2) Utawala wa Rwanda ni jamhuri.
3) Kiongozi mkuu wa Rwanda ni rais.
4) Utawala wa utungaji wa sheria, Utawala wa kiutendaji na utawala wa kisheria.
5) Wanyarwanda husemekana kuwa wachapakazi kwa sababu wanapenda kufanya kazi ili kuiendeleza nchi yao. Kila mwishoni mwa nwezi hufanya msaragambo.
6) **Viongozi wa kuchagulia:** rais, wabunge, maseneta ( baadhi yao), meya, wakuu wa vitongoji.

   **Viongozi wa kuteuliwa:** magavana, mawaziri, maseneta (baadhi yao), mwendeshamashtaka mkuu wa serikali na jaji mkuu.

**Wanaopitia katika mitihani:** waendeshamashtaka, majaji, makatibu watendaji wa tarafa na kata.

**Msamiati kuhusu kifungu cha habari**

***Kazi ya 3: Kazi hii ni ya mwanafunzi binafsi. Mkufunzi awaelekeze wanafunzi katika kutoa maana za maneno. Mkufunzi ahakikishe kwamba kila mwanafunzi amefanya kazi kisha asahihishe majibu ya wanafunzi. Yafuatayo ni majibu yaliyopendekezwa:***

- **Jamhuri**: Nchi huru inayotawaliwa na rais wa kuchaguliwa na wananchi.
- **Kura**: Uchaguzi.
- **Kuteuliwa**: Kuchukuliwa miongoni mwa vitu zaidi ya kimoja.
- **Majimbo**: Sehemu za nchi zilizo kubwa kuliko wilaya.
- **Halmashauri**: Kikundi cha watu maalum walioteuliwa au kuchaguliwa kuelekeza jambo.

***Kazi ya 4: Kazi hii ni ya mwanafunzi binafsi. Mkufunzi akakikishe kuwa kila mwanafunzi anafanya kazi vilivyo. Yafuatayo ni majibu:***

1 (e), 2 (d), 3 (b), 4 (b), 5 (a)

**Sarufi: Matumizi ya ngeli ya PA-M-KU**

***Kazi ya 5: Kazi hii ifanyiwe katika jozi. Mkufunzi ahakikishe kuwa kila jozi inawajibika vilivyo. Yafuatayo ni majibu yaliyopendekezwa:***

- Haya ni majina ya ngeliya PA,M,KU. Majina haya yamepachikwa kiambishi **-ni** mwishoni mwa majina ya kawaida ili kupata majima ya ngeli hii.

***Kazi ya 6: Kazi hii iwe ya kibinafsi ili kujenga tabia ya kujitegemea kwa wanafunzi.***

1) M-Ku-
2) Ku-
3) Pa-
4) M-

**Kazi ya 7:** ***Kazi hii ifanyiwe katika jozi. Mkufunzi ahamasishe wanafunzi wawili wawili kushirikiana na kujibu kazi waliyopewa. Yafuatayo ni majibu yaliyopendekezwa:***

a) Kupi: Kivumishi cha kuuliza
b) Papi: Kivumishi cha kuuliza
c) Hapa: Kivumishi cha kuonyesha
d) Mwa: kivumishi cha a-unganifu
e) Penyewe:kivumishi cha kurejesha
f) Humu:kivumishi cha kuonyesha

g) Kwetu: kivumishi cha kumiliki
h) Hapa: kivumishi cha kuonyesha
i) Mwangu: kivumishi cha kumiliki

**Kazi ya 8:** ***Kazi hii iwe ya kibinafsi na mkufunzi ahakikishe kwamba amesahihisha majibu ya kila mwanafunzi. Yafuatayo ni majibu:***

a) Mle
b) Kwetu
c) Huku
d) Kuzuri
e) Mwangu
f) Mwenyewe
g) Mwa
h) Papi
i) Penyewe
j) Kwa

**Matumizi ya lugha: Maelezo muhimu kuhusu msamiati katika maeneo ya utawala**

**Kazi ya 9:** ***Kazi hii ifanyike kwa makundi madogo madogo. Kazi hii ina lengo la kupanua msamiati wa mwanafunzi. Mkufunzi ahakikishe kuwa kila kundi linafanya kazi vilivyo.***

***Majibu :***

1) Taifa ni jamii ya watu wanaoishi katika nchi moja na wanaounganika kutokana na matukio ya kihistoria lakini jamhuri ni nchi huru inayotawaliwa na rais wa kuchaguliwa na wananchi.
2) Ufalme ni utawala wa mfalme au eneo ambalo liko chini ya mamlaka ya mfalme lakini jamhuri ni nchi huru inayotawaliwa na rais wa kuchaguliwa na wananchi. Ufalme ni wa kurithiwa lakini rais huchaguliwa na wananchi.
3) Katiba ni jumla ya kanuni ambazo kwazo huwezesha serikali itawale au chama au kampuni iendeshe shughuli zake.

**Kusikiliza na kuzungumza**

**Kazi ya 10:** ***Kazi hii ni ya mwanafunzi binafsi na baadaye ni kazi ya makundi madogo madogo. Mkufunzi ahakikishe kwamba kila mwanafunzi amesikiliza taarifa ya habari na kujadiliana na wenzake.***

**Kuandika**

**Kazi ya 11:** ***Kazi hii ni ya wanafunzi binafsi. Ni ya kutunga mazungumzo akibainisha msamiati kuhusu maeneo ya utawala, akitilia mkazo kwenye matumizi ya majina ya ngeli ya PA-M-KU. Mkufunzi ahakikishe kuwa kila mwanafunzi amefanya kazi vilivyo.***

## 1.6. Kazi ya utafiti


Katika makundi yao, wanafunzi wafanye utafiti kuhusu msamiati wa ngazi za utawala za hapa Rwanda kabla ya mauaji ya kimbali dhidi ya Watutsi mnamo mwaka wa 1994.

## 1.7. Muhtasari wa mada

Mada hii ya kwanza "**MATUMIZI YA KISWAHILI KATIKA MAENEO YA UTAWALA**" ina somo moja linalohusiana na mada husika. Somo hili lina vipengele vidogo vidogo kama vile: kifungu cha habari, maswali ya ufahamu, matumizi ya msamiati, sarufi, matumizi ya lugha, kusikiliza na kuzungumza na kuandika. Somo hili lilipewa kichwa cha "**Nchi yetu Rwanda.**"

## 1.8. Maelezo ya ziada kwa mkufunzi

- Nchi: Ni sehemu ya ardhi katika ulimwengu iliyogawanyika kisiasa kwa mipaka na kutambulikana kwa taifa lake.
- Taifa: Ni jamii ya watu wanaoishi katika nchi moja na wanaounganika kutokana na matukio ya kihistoria.
- Taifa lisilokuwa jamhuri huitwa ufalme.
- Nchi huru inaongozwa na katiba.
- Rwanda ni nchi, taifa na jamhuri. Uongozi wa Rwanda unaonyeshwa na kielelezo kifuatacho:



1) Katika maisha ya Wanyarwanda, watu wanaoishi Rwanda au watu wanaotembelea nchini Rwanda hupewa vitambulisho mbalimbali. Vitambulisho hivyo ni kama vile kitambulisho cha uraia, kadi ya uchaguzi, kadi ya ukimbizi, leseni ya kuongoza magari na pikipiki na kadhalika.

2) Katika maisha yao, Wanyarwanda hupumzika na kuhuzunika na hasa kujiburudisha ndiyo maana nchini Rwanda kuna sikukuu mbalimbali na siku maalum. Miongoni mwa sikukuu hizi kuna zile za kimataifa (sikukuu ya kazi, ya wanawake,...) na nyingine za kitaifa (Sikukuu ya Uhuru, sikukuu ya Ukombozi, ...). Siku maalum ni kama tarehe 7 Aprili wakati ambapo Wanyarwanda hukumbuka waliouawa wakati wa mauaji ya kimbari dhidi ya Watutsi yaliyotokea mnamo mwaka wa 1994.

**Baadhi ya tarehe, siku maalum na sikukuu au sherehe husika:**

1) Tarehe (ya kwanza/mosi) Januari kila mwaka: Sikukuu ya mwaka mpya.
2) Tarehe 1 Februari: Sikukuu ya Mashujaa wa Taifa.
3) Tarehe 14 Februari: Sherehe ya wapendanao.
4) Tarehe 8 Machi: Sikukuu ya wanawake.
5) Tarehe 22 Machi: Sikukuu ya maji duniani.
6) Tarehe 7 Aprili: Siku ya maombolezo nchini Rwanda. Ni siku ya kumbukumbu ya mauaji ya kimbari dhidi ya Watutsi mnamo mwaka wa 1994.
7) Tarehe 1 Mei: Sikukuu ya kazi duniani.
8) Tarehe 5 Juni: Sikukuu ya mazingira.
9) Tarehe 16 Juni: Sikukuu ya Mtoto wa Afrika
10) Tarehe 1 Julai: Sikukuu ya Uhuru.
11) Tarehe 4 Julai: Sikukuu ya kujikomboa (ukombozi).
12) Ijumaa ya kwanza ya mwezi Agosti: Sherehe ya mavuno (Sikukuu ya Umuganura).
13) Tarehe 21 Septemba: Sherehe ya Amani.
14) Tarehe 9 Oktoba: Sherehe ya walemavu.
15) Tarehe 25 Desemba kila mwaka: Sikukuu ya Krismasi.

**TNBH:** Siku maalum na sikukuu ni nyingi sana. Kuna zisizobadilika na zinazobadikila (Idi, Raidi kubwa, Pasaka).

## 1.9. Tathmini ya mada

*Hii ni kazi ya kupima maarifa, ufahamu na stadi ambazo mwanafunzi amepata kutokana na yale aliyojifunza katika mada husika. Baada ya wanafunzi kufanya tathmini hii, mkufunzi asahihishe hadharani kazi yote ili wanafunzi waweze kujua makosa ambayo wameyafanya.*

1) Nyanja tatu za uongozi wa Rwanda ni utawala wa utungaji wa sheria, utawala wa kiutendaji na utawala wa kisheria

2) Aina tano za vitambulisho vinavyoweza kupatikana nchini Rwanda ni kitambulisho cha uraia, kadi ya uchaguzi, kadi ya ukimbizi, leseni ya kuongoza magari au pikipiki, kadi ya bima, kadi ya kazi, kadi ya shule, n.k.

3) Majina ya:

    - viongozi wa kuchaguliwa ni rais, wabunge, maseneta (baadhi yao), meya,
    - viongozi wa kuteuliwa ni magavana, mawaziri, maseneta (baadhi yao), mwendeshamashtaka mkuu wa serikali, jaji mkuu,
    - wanaopitia katika mitihani waendeshamashtaka, majaji, makatibu watendaji wa tarafa na kata.

4) Ufalme ni utawala wa mfalme au eneo (nchi) ambalo liko chini ya mamlaka ya mfalme lakini jamhuri ni nchi huru inayotawaliwa na rais wa kuchaguliwa na wananchi. Ufalme ni wa kurithiwa kakini rais huchaguliwa na wananchi.

5) Rwanda ni jamhuri kwa sababu inatawaliwa na rais.

## 1.10. Kazi za ziada

### 1.10.1. Kazi za urekebishaji

**Kazi ya 1:** ***Husisha viongozi wafuatao na ngazi za uongozi zifuatazo:***

| KIONGOZI | NGAZI YA UONGOZI |
|---|---|
| 1) Meya | i) Jimbo |
| 2) Katibu mtendaji wa Tarafa | ii) Wilaya |
| 3) Gavana | iii) Kata |
| 4) Katibu Mtendaji wa Kata | iv) Tarafa |

**Jibu:** 1 (ii), 2 (iv), 3 (i), 4 (iii)

### 1.10.2. Kazi jumuishi

**Kazi ya 2:** ***Taja nchi zinazopakana na Rwanda*.**

**Jibu:** Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Jamhuri ya Burundi, Jamhuri ya Uganda na Jamhuri ya Kidemokarasia ya Kongo,

**Kazi ya 3:**

- ***Ni kitambulisho gani kinachohitajika wakati ambapo mtu anataka kutoka nje ya nchi?***
- ***Ni nini chanzo cha sikukuu ya mtoto wa Afrika?***

**Majibu***:*

- Pasipoti
- Chanzo cha sikukuu ya mtoto wa Afrika ni mauaji ya watoto weusi yaliyofanywa na wazungu katika jimbo la Soweto katika Jamhuri ya Afrika Kusini wakati wa Ubaguzi wa Rangi.

### 1.10.3. Kazi za nyongeza

**Kazi ya 4:** ***Wewe ni raia wa kawaida na umepoteza kitambulisho cha uraia. Umekwenda kwenye kituo cha polisi kuomba kitambulusho kingine, tunga mazungumzo kati yako na askali polisi.***

MADA YA
2

# KISWAHILI NA FASIHI SIMULIZI

## 2.1. Uwezo mahususi

- Kufafanua kwa kina dhana ya fasifi simulizi
- Kusoma na kusimulia hadithi za masimulizi
- Kubainisha aina za maneno

## 2.2. Ujuzi wa awali

Kupitia masomo waliyofundishwa katika lugha nyingine (Kinyarwanda, Kiingereza na fasihi ya Kiingereza) wanafunzi hawa wana ujuzi wa jumla kuhusu fasihi simulizi. Lakini ujuzi huu haukamiliki kwa sababu ni mara ya kwanza wanafunzi hawa kusoma fasihi hasa fasihi simulizi katika lugha ya Kiswahili.

## 2.3. Masuala mtambuka katika mada

Katika masomo ya mada hii kwenye vifungu, michoro au picha, utumiaji wa msamiati katika sentensi, matumizi ya lugha, kuandika, kuzungumza na katika mazoezi au kazi na sarufi; mkufunzi anawaongoza wanafunzi katika ujifunzaji na kutumia maswala mtambuka yafuatayo:

**i) Mafunzo kuhusu amani na maadili mema**

a) Katika majadiliano, wanafunzi hutarajiwa kutokasirika ovyo na kusikiliza wengine wakitoa hoja zao. Majadiliano haya huwafundisha wahusika kusikilizana na kuelewana kama njia mojawapo ya kujenga amani imara na kuchukua uamuzi mmoja.

b) Kwa kutunga sentensi, mkufunzi awaongoze kutunga sentensi zenye mafunzo yanayohusu amani na maadili mema.

**ii) Mafunzo kuhusu desturi ya usanifishaji**

Kwa kufanya kazi yoyote, ama kuandika inafaa kuchunguza kama unafuata taratibu za kuandika.

**iii) Elimu jumuishi**

Makundi ya wanafunzi wenye mahitaji maalumu ya kielimu kama vile: wanafunzi wenye matatizo ya ulemavu, wanafunzi wenye kipaji maalumu katika uwezo wa kujifunza, na kadhalika washughulikiwe ipasavyo.

Kumbuka kuwa wanafunzi wenye matatizo kama haya ni kama wengine; walikuja shuleni ili wapate maarifa na maadili yanayotakiwa. Kwa hiyo, ni lazima wewe mkufunzi uwasaidie ipasavyo.

**iv) Mazingira na maendeleo endelevu**

Mkufunzi, kupitia mazoezi ya msamiati na sarufi, anaweza kueleza umuhimu wa kuhifadhi mazingira kwa maisha ya watu.

**v) Usawa wa jinsia**

1) Mwalimu katika mifano yote, ni lazima kutoa mifano inayoonyesha usawa wa jinsia;

2) Katika mazoezi ya kutunga sentensi, ni vizuri kutunga sentensi ambazo zinaeleza na zinatoa maelezo kuhusu usawa wa jinsia;

3) Kazi katika makundi, ni vizuri kupanga wasichana na wavulana katika kundi moja ili darasani pasiwe na kundi la jinsia moja.

**vi) Elimu kuhusu uzalishajimali/ujasiriamali**

Katika kazi na mazoezi ambayo mkufunzi atawapangia wanafunzi kutakuwa na suala mtambuka hili. Wanafunzi watapewa fursa ya kufikiria na kuzungumzia kuhusu suala hili kwa sababu masomo yote wanayoyasoma ni ya kuwazindua ili wajitegemee nyakati zijazo.

## 2.4. Mwongozo kuhusu kazi ya utangulizi wa mada

- Kwa kutangulia mada, mkufunzi atauliza maswali ambayo yatawasaidia wanafunzi kufunua mada hii;
- Wanafunzi wanaweza kushindwa kutoa majibu sahihi mwanzoni, lakini wanaweza kufanikiwa kwa kupitia masomo tofauti, mazoezi, vifungu, na kazi nyingine zilizotaarishwa kwenye mada hii.

## 2.5. Orodha ya masomo na tathmini

| Kichwa cha somo | Malengo ya kujifunza | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|
| **1. Dhana ya fasihi simulizi** | **Maarifa na ufahamu:** Kufafanua msamiati kuhusu fasihi simulizi<br>**Stadi**: Kutumia msamiati kuhusu fasihi simulizi katika sentensi na matini.<br>**Maadili na mwenendo mwema:** Kufurahia fasihi simulizi na kujihiia hamu ya kuiga mazuri katika kazi za sanaa au fasihi. | 3 |
| **2. Hadithi** | **Maarifa na ufahamu:** Kueleza maana ya hadithi<br>**Stadi:** Kutunga hadithi<br>**Maadili na mwenendo mwema:** Kuitumia hadithi kwa malengo chanya na kuepuka matumizi mabaya ya hadithi | **3** |
| **Tathmini ya mada** | | **1** |
| **Vipindi vyote vya mada ya 2** | | **7** |

# SOMO LA 2: DHANA YA FASIHI SIMULIZI

## a) Malengo ya ujifunzaji

Kabla ya somo hili kutiliwa nanga mwanafunzi atakuwa akiweza:

- Kueleza maana ya fasihi
- Kutaja tanzu za fasihi
- Kuonyesha umuhimu wa fasihi simulizi
- Kutaja vipengele vya fasihi simulizi
- Kukuza na kuhifadhi utamaduni, mila na desturi kupitia vipengele vya fasihi simulizi
- Kubaini na kuonyesha aina za maneno.

## b) Zana za Kujifunzia

Ili somo liweze kufika kwenye malengo yake, ni lazima mkufunzi ajaribu kutafuta zana za ufundishaji zitakazomsaidia kufanikisha somo lake ili kukidhi mahitaji ya wanafunzi na malengo ya somo husika. Katika somo hili zana muhimu ni:

- Kitabu cha mwanafunzi,
- Mwongozo wa mkufunzi,
- Michoro mbalimbali,
- Ubao,
- Chaki na vifaa vinavyoweza kuwasaidia wanafunzi kuelewa somo akitilia mkazo kuhusu hali za wanafunzi wanaohitaji uangalifu maalum kama wanafunzi wenye ulemavu mbalimbali.

Vifaa hivi vitaandaliwa kulingana na mazingira ya shule. Kwa hiyo, mkufunzi anaweza kuandaa vifaa kadhaa viwezavyo kumsaidia kufanikisha somo. Ikiwezekana, hakikisha kuwa kuna vifaa kwa wanafunzi wenye mahitaji maalumu. Unapowapa wanafunzi kazi mbalimbali, hakikisha kuwa wanafunzi wenye mahitaji maalumu wamepewa kazi tofauti zitakazowawezesha kupata ujuzi uliokusudiwa. Baadhi ya wanafunzi wenye matatizo ya kiakili huenda wasiweze kuchora lakini wakawa na uwezo wa kutumia rangi mbalimbali chini ya usaidizi wako au wenzao. Mkufunzi anapaswa kuwa mbunifu ndiyo sababu yeye mwenyewe ajibunie vifaa visaidizi mbalimbali.

**c) Ujuzi wa awali/Marudio/Utangulizi**

Somo hili linajishughulisha na dhana ya fasihi simulizi. Mkufunzi aanze somo kwa kuwaamkia wanafunzi. Wanafunzi watajibu maamkizi ya mkufunzi kisha atangulize somo kwa kuwauliza maswali mepesi ya kuwachangamsha. Maswali haya yanapaswa kuwa na uhusiano na somo jipya.

Mkufunzi atakachofanya ni kuwashirikisha wanafunzi wake ili waweze kuwasiliana kuhusu fasihi, kisha atafanya chochote ili awawezeshe wanafunzi kufika kwenye kile anachotaka kufundisha.

**d) Maelekezo kuhusu kazi za ujifunzaji**

Katika hatua hii, mkufunzi atatafuta mbinu mbalimbali zitakazomwezesha kufika kwenye malengo ya somo lake. Katika somo hili, mkufunzi atatilia mkazo kwenye:

- **Utumiaji wa makundi ya wanafunzi**: Kwa sababu mwanafunzi ndiye kiini cha ufundishaji na ujifunzaji ni lazima mbinu itumiwe ili kumushirikisha mwanafunzi katika mambo yote yanayofanyiwa darasani. Wanafunzi watatumia makundi yao kwa kufanya kazi zote watakazopewa na mkufunzi na zile zipatikanazo katika kitabu cha wanafunzi.
- **Fikiri-Jozi-Changia:** Mbinu hii itatumiwa mahali ambapo kazi inaomba kufanyika kwa jozi.
- **Kazi binafsi kwa wanafunzi**: Itakuwa lazima kila mwanafunzi apewe kazi/mazoezi yake binafsi (kwa mfano: kusoma kifungu cha habari, kufanya majaribio, mitihani mbalimbali na hata kazi za nyumbani).
- **Maswali na majibu**: Mara nyingi somo huwa na majadiliano kati ya mwalimu na wanafunzi. Kuhusiana na mbinu hii, mkufunzi atawauliza wanafunzi maswali mbalimbali nao watajibu maswali hayo. Vilevile wanafunzi kwa upande wao wanaweza kumwuliza mkufunzi maswali kadhaa naye akawajibu. Tena maswali na majibu haya yanaweza kuwa kati ya wanafunzi wenyewe.
- **Maelezo ya mkufunzi**: Mbali na kuwa mwanafunzi hupewa kipaumbele katika somo, mkufunzi angali msuruhifu katika somo lake. Kwa hiyo, mkufunzi atatumia mbinu hii kwa kueleza mambo yatakayohitaji maelezo yake ili kufanikisha somo lake.

**Kidokezo**

***Haya ni maswali ya kumwingiza mwanafunzi katika somo hili kwa urahisi. Ni maswali yanayoamsha upekuzi au udadisi.***

**e) Majibu:**

**Kazi ya 1:** ***Mkufunzi aweke wanafunzi katika makundi madogo madogo kisha awaombe kuchunguza na kueleza shughuli zinazoendelea kwenye michoro husika.***

**Kusoma na ufahamu: Dhana ya fasihi na umuhimu wake**

**Kazi ya 2:** ***"Kusoma na ufahamu" ni mojawapo ya stadi zinazotarajiwa kwa mwanafunzi wa lugha. Usomaji mzuri wa kifungu husaidia kukifahamu, na ndiyo sababu mkufunzi anapaswa kuwasaidia wanafunzi wanaposoma kifungu kwa kuzingatia matamshi bora ya maneno, hasa maneno mapya, matumizi ya alama za uakifishaji, n.k.***

***Maswali haya ya ufahamu yafanyiwe katika makundi madogo madogo. Wanapojibu maswali ya ufahamu, wanafunzi wanatarajiwa kutunga sentensi nzima, siyo neno moja tu. Wasimamizi wa baadhi ya makundi wawasilishe majibu yao darasani. Yafuatayo ni majibu ya maswali ya ufahamu yaliyopendekezwa.***

1) Fasihi ni kazi ya sanaa inayomulika hisi mwazo na malengo ya jamii kwa kutumia lugha.
2) Kuna tanzu kubwa za fasihi: fasihi simulizi na fasihi andishi.
3) Vipera vya fasihi simulizi ni kama vile hadithi, methali, nahau, misemo, vitendawili.
4) Kioo ni kifaa cha kujitazamia. Kulingana na hili fasihi husaidia wanajamii kuona kasoro zao na wakaweza kujirekebisha.
5) Fasihi ina umuhimu wa kuelimisha jamii, kuonya jamii, kulinda jamii, kuburudisha jamii, n. k.

**Msamiati kuhusu kifungu cha habari**

**Kazi** *ya* **3:** ***Kazi hii ni ya mwanafunzi binafsi. Mkufunzi awaelekeze wanafunzi katika kutoa maana za maneno. Mkufunzi ahakikishe kwamba kila mwanafunzi amefanya kazi kisha asahihishe majibu ya wanafunzi. Yafuatayo ni majibu yaliyopendekezwa:***

1) **Mkoba**: mfuko mdogo uliosukwa au uliotengenezwa kwa ngozi na unaotumiwa kutilia vitu.
2) **Akitabasamu**: akionyesha uso wa furaha unaoambatana na haja ya

kucheka bila ya kutoa sauti wala kufungua mdomo.

3) **Mcheshi**: mtu mwenye tabia kuchekesha kwa mazungumzo yenye porojo

4) **Itikadi**: imani

5) **Kujiandaa**: kujitayarisha

**Kazi ya 4:** *Kazi hii ni ya mwanafunzi binafsi. Mkufunzi awaelekeze wanafunzi katika kujaza mapengo. Mkufunzi ahakikishe kwamba kila mwanafunzi amefanya kazi kisha asahihishe majibu ya wanafunzi. Yafuatayo ni majibu:*

1) Itikadi
2) Ilhali
3) Enzi
4) Hulenga
5) Tamasha

**Sarufi: Aina za maneno**

**Kazi ya 5:** ***Kazi hii ifanyiwe katika makundi madogo madogo. Mkufunzi ahakikishe kuwa kila kundi linafanya vilivyo. Yafuatayo ni majibu***

a) Aina za maneno yaliyotumiwa:
- **Mheshimiwa**: jina lakawaida
- **Rais**: jina la kawaida
- **Jamii**: jina la makundi
- **Wanyarwanda**: jina la pekee
- **Watu**: jina la kawaida

b) Kila kundi litatunga sentensi za aina yake. Zifuatazo ni sentensi pendekezi
- **Ni**: Mutesi **ni** mwanafunzi
- **Mkisoma**: **Mkisoma** vizuri mtashinda.
- **Palilia**: Mkulima **anapalilia** mahindi
- **Sambaza**: Ni vizuri kunawa mikono kwa **kutosambaza** magonjwa.
- **Utakuwa**: Usiku wa leo **utakuwa** mzuri sana.

**Matumizi ya lugha: Dhana ya fasili na umuhimu wake**

**Kazi ya 6:** ***Kazi hii ifanyike katika makundi madogo madogo. Mkufunzi ahakikishe kwamba wanafunzi wanafanya kazi kufuatana na maagizo. Yafuatayo ni majibu kuhusu maelezo muhimu:***

1) Fasihi ni kazi ya Sanaa imulikayo hisi, mawazo na malengo ya jamii kwa kutumia lugha.

2) Fsihi ina umuhimu wa kuelimisha jamii, kuburudisha jamii, kuonya jamii, kuelekeza jamii, kuhifadhi utamaduni, kulinda utamaduni, kukuza lugha, kuunganisha watu, …

3) Fasihi ya Kiswahili ni aina ya fasihi inayohusu jamii ya waswahili lakini fasiki katika Kiswahili ni fasihi ya jamii yoyote ile iliyoandikwa kwa lugha ya Kiswahili.
4) Vipera vya fasihi simulizi ni kama vile hadithi, methali, nahau, misemo, vitendawili na ushairi.

**Kusilikiza na kuzungumza**

**Kazi ya 7:** ***Kazi hii ifanyike kwa jozi. Kila kundi litafute, litege na litegue vitendawili hadharani. Mkufunzi ahakikishe kwamba wanafunzi wanafanya kazi kwa kufuata maagizo.***

**Kuandika**

**Kazi ya 9:** ***Kazi hii ni ya mwanafunzi binafsi. Huyu analazimishwa kutunga insha. Mkufunzi ahakikishe kwamba kila mwanafunzi anaandika vilivyo kuhusiana na mada.***

# SOMO LA 3: HADITHI

### a) Malengo ya ujifunzaji

Kabla ya somo hili kutiliwa nanga mwanafunzi atakuwa akiweza:

- Kueleza maana ya hadithi
- Kutaja tanzu za hadithi
- Kuonyesha umuhimu wa hadithi
- Kusimulia hadithi
- Kukuza na kuhifadhi utamaduni, mila na desturi kupitia hadithi
- Kubaini na kuonyesha aina za maneno

### b) Zana za Kujifunzia

Ili somo liweze kufika kwenye malengo yake, ni lazima mkufunzi ajaribu kutafuta zana za ufundishaji zitakazomsaidia kufanikisha somo lake ili kukidhi mahitaji ya wanafunzi na malengo ya somo husika. Katika somo hili zana muhimu ni:

- Kitabu cha mwanafunzi,
- Mwongozo wa mkufunzi,
- Michoro mbalimbali,
- Ubao,
- Chaki na vifaa vinavyoweza kuwasaidia wanafunzi kuelewa somo akitilia mkazo kuhusu hali za wanafunzi wanaohitaji uangalifu maalum kama wanafunzi wenye ulemavu mbalimbali.

Vifaa hivi vitaandaliwa kulingana na mazingira ya shule. Kwa hiyo, mkufunzi anaweza kuandaa vifaa kadhaa viwezavyo kumsaidia kufanikisha somo. Ikiwezekana, hakikisha kuwa kuna vifaa kwa wanafunzi wenye mahitaji maalumu. Unapowapa wanafunzi kazi mbalimbali, hakikisha kuwa wanafunzi wenye mahitaji maalumu wamepewa kazi tofauti zitakazowawezesha kupata ujuzi uliokusudiwa. Baadhi ya wanafunzi wenye matatizo ya kiakili huenda wasiweze kuchora lakini wakawa na uwezo wa kutumia rangi mbalimbali chini ya usaidizi wako au wenzao. Mkufunzi anapaswa kuwa mbunifu ndiyo sababu yeye mwenyewe ajibunie vifaa visaidizi mbalimbali.

**c) Ujuzi wa awali/Marudio/Utangulizi**

Somo hili linajishughulisha na hadithi kama kipera cha fasihi simulizi. Mkufunzi aanze somo kwa kuwaamkia wanafunzi. Wanafunzi watajibu maamkizi ya mkufunzi kisha atangulize somo kwa kuwauliza maswali mepesi ya kuwachangamsha. Maswali haya yanapaswa kuwa na uhusiano na somo jipya.

Mkufunzi atakachofanya ni kuwashirikisha wanafunzi wake ili waweze kuwasiliana kuhusu fasihi, kisha atafanya chochote ili awawezeshe wanafunzi kufika kwenye kile anachotaka kufundisha.

**d) Maelekezo kuhusu kazi za ujifunzaji**

Katika hatua hii, mkufunzi atatafuta mbinu mbalimbali zitakazomwezesha kufika kwenye malengo ya somo lake. Katika somo hili, mkufunzi atatilia mkazo kwenye:

- **Utumiaji wa makundi ya wanafunzi**: Kwa sababu mwanafunzi ndiye kiini cha ufundishaji na ujifunzaji ni lazima mbinu hii itumiwe ili kumushirikisha mwanafunzi katika mambo yote yanayofanyiwa darasani. Wanafunzi watatumia makundi yao kwa kufanya kazi zote watakazopewa na mkufunzi na zile zipatikanazo katika kitabu cha wanafunzi.
- **Fikiri-Jozi-Changia:** mbinu hii itatumiwa mahali ambapo kazi inaomba kufanyika kwa jozi.
- **Kazi binafsi kwa wanafunzi**: Itakuwa lazima kila mwanafunzi apewe kazi/mazoezi yake binafsi (kwa mfano: kusoma kifungu cha habari, kufanya majaribio, mitihani mbalimbali na hata kazi za nyumbani).
- **Maswali na majibu**: Mara nyingi somo huwa na majadiliano kati ya mkufunzi na wanafunzi. Kuhusiana na mbinu hii, mkufunzi atawauliza wanafunzi maswali mbalimbali nao watajibu maswali hayo. Vilevile, wanafunzi kwa upande wao wanaweza kumwuliza mkufunzi maswali kadhaa naye akawajibu. Tena maswali na majibu haya yanaweza kuwa kati ya wanafunzi wenyewe.
- **Maelezo ya mkufunzi**: Mbali na kuwa mwanafunzi hupewa kipaumbele katika somo, mkufunzi angali mwezeshaji katika somo lake. Kwa hiyo, mkufunzi atatumia mbinu hii kwa kueleza mambo yatakayohitaji maelezo yake ili kufanikisha somo lake.

**e) Majibu:**

**Kazi ya 1:** *Haya ni maswali ya kumwingiza mwanafunzi katika somo hili kwa urahisi. Ni maswali yanayoamsha upekuzi au udadisi. Ni ya kujibiwa akilini mwa mwanafunzi. Si kazi inayohitaji utafiti wowote. Mwanafunzi akiyasoma atakuwa na fursa ya kujua kusudi la somo. Hali kadhalika, hii ni kazi itakayomsaidia mkufunzi kutangulia somo kwa urahisi. Wanafunzi wapewe muda wa kusoma maswali hayo. Mapendekezo ya jibu.*

Mchoro huu unaonyesha aina mbalimbali za wanyama walio mkutanoni.

**Kusoma na ufahamu: Wafalme wawili**
**Kazi ya 2:** ***"Kusoma na ufahamu" ni mojawapo ya stadi zinazotarajiwa kwa mwanafunzi wa lugha. Usomaji mzuri wa kifungu husaidia kukifahamu, na ndiyo sababu mkufunzi anapaswa kuwasaidia wanafunzi wanaposoma kifungu, kwa kuzingatia matamshi bora ya maneno, hasa maneno mapya, matumizi ya alama za uakifishaji, n.k.***

***"Wafalme wawili" ni kifungu. Inapendekezwa kisomewe katika makundi. Mkufunzi awe makini ili asahihishe makosa ya kusoma yanayoweza kujitokeza.***

***Maswali haya ya ufahamu yafanyiwe katika makundi madogo madogo. Wanapojibu maswali ya ufahamu wanafunzi wanatarajiwa kutunga sentensi nzima, siyo neno moja tu. Wasimamizi wa baadhi ya makundi wawasilishe majibu yao darasani. Yafuatayo ni majibu ya maswali ya ufahamu yaliyopendekezwa:***

1) Ni kwa sababu wanyama hao hawakuwa na mfalme, na walipotazama kwenye misitu mingine, waliona kwamba wanyama wengine wana wafalme, wakafikiri kwamba wanyama hao wana maisha bora kuliko wao kisha wakajichagulia mfalme.

2) Wanyama waliohudhuria mkutano wa kuchagua mfalme ni:Bwana Nguruwe, Simba,Tembo, Chui, Twiga, Ngiri, Sungura, Nguchiro, Fisi, Nyoka, Mbogo, ndege wote na samaki.

3) Alipewa fursa ya kuelezea wanyama wengine sababu yeye ndiye anapaswa kuchaguliwa kuwa mfalme, huku akijaribu kufahamisha kwamba yeye ana tabia nzuri nyingi zaidi kushinda wanyama wengine

4) Alisema maneno yaliyopendwa na wanyama wengine, akisema kuwa akichaguliwa kuwa mfalme wao, atalinda usalama wao, mabibi zao na watoto wao. Hakutakuwa na mnyama kutoka misitu mingine atakayewashambulia. Hata binadamu hataingia hapo tena.

5) Aliwaambia kuwa kazi ya kulinda usalama wao ni kazi ngumu sana na inamlazimisha kula chakula kizuri kila siku. Akawaambia “Mimi sitaendelea kula nyasi kuanzia leo. Hiyo inamaanisha kwamba kila siku ninahitaji wanyama watakaoniletea chakula ili nile vizuri!”

**Msamiati kuhusu "Wafalme wawili"**

**Kazi ya 3:** ***Kazi hii ni ya mwanafunzi binafsi. Mkufunzi awaelekeze wanafunzi katika kutoa maana za maneno. Mkufunzi ahakikishe kwamba kila mwanafunzi amefanya kazi kisha asahihishe majibu ya wanafunzi. Yafuatayo ni majibu yaliyopendekezwa:***

1) **Mfalme**: Kiongozi, mtawala wa kiume aliyepata nguvu za utawala kwa njia ya urithi au uwezo fulani k. v. ushujaa.
2) **Uhuru**: Hali ya kutotawaliwa na mtu au nchi nyingine, hali ya kufanya mambo bila ya kuingiliwa.
3) **Kuwashawishi**: Kuwafanya watu wavutike kutenda jambo fulani.
4) **Tegeni masikio**: Sikilizeni.
5) **Alijiuzulu**: Aliacha madaraka yake kwa hiari.

**Sarufi: Aina za maneno ya Kiswahili**

**Kazi ya 4:** ***Kazi hii ifanyike kwa jozi na kuchunguza maneno yaliyopigiwa mistari.. Mkufunzi ahakikishe kuwa kila kundi linafanya kazi vilivyo. Yafuatayo ni majibu:***

***Vivumishi hivyo ni:*** *kubwa, bora, zuri, la, maovu, ile, yule, hicho, gani?*

**Kazi ya 5:** ***Kazi hii ifanyike kwa jozi. Mkufunzi ahakikishe kuwa kila kundi linafanya kazi kufuatana na maagizo.***

**Viwakilishi hivyo ni:** haya, lipi, u-, wengine, wa-, chochote, a-, wengi, wa, huko, mingapi.

**Matumizi ya lugha: Maelezo muhimu kuhusu hadithi**

**Kazi ya 6:** ***Kazi hii ifanyiwe katika makundi madogo madogo na baadaye wanafunzi wajibu maswali yatakayofuata. Mkufunzi ahakikishe kuwa kila kundi linawajibika vilivyo.***

**Majibu:**

1) Hadithi ni mambo ya kubuni huwa yanaeleza ukweli katika jmii.
2) Katika Kiswahili kuna hadithi ambazo ni hekaya, hurafa, ngano, mighani, visasili

3) Tunatumia wanyama katika hadithi ili kujiepusha na ugomvi.

4) Hekaya ni hadithi ambayo wahusika wake ni binadamu tu ilhali mighani ni hadithi zinazohusu ushujaa.

5)

| **Mnyama** | **Tabia** |
|---|---|
| Simba | Kiongozi |
| Fisi | Mwoga/ mroho |
| Sungura | Mjanja |
| Chui | Mharibifu |
| Nyani | Mwenye busara |
| Tembo | Kimbelembele |
| Kinyonga | Kigeugeu |

**Kusikiliza na kuzungumza**

**Kazi ya 7:** ***Kazi hii ni ya mwanafunzi binafsi. Huyu atasimulia hadithi moja anayoifahamu kwa kuzingatia mianzo na miisho ya hadithi za kimapokeo kama zilivyoonyeshwa hapo juu. Mkufunzi ahakikishe kuwa kila mtu anawajibika vilivyo. Mkufunzi anaombwa kusahihisha makosa ya kimatamshi au kisarufi yatakayoweza kujitokeza.***

**Kuandika**

**Kazi ya 8:** ***Kazi hii ni ya mwanafunzi binafsi. Huyu anatakiwa kuandika hadithi moja anayoifahamu kutoka katika jamii ya Rwanda kwa kuzingatia mianzo na miisho ya hadithi za kimapokeo kama zilivyoonyeshwa. Mkufunzi ahakikishe kuwa kila mtu amewajibika vilivyo. Tena, mkufunzi anaombwa kusahihisha makosa ya kimaandishi yatakayoweza kujitokeza.***

## 2.6. Kazi ya utafiti

Katika makundi yao, wanafunzi wafanye utafiti kuhusu sababu za kudidimia kwa fasihi simulizi, kisha wawasilishe darasani.

## 2.7. Muhtasari wa mada

Mada hii ya pili "**KISWAHILI NA FASIHI SIMULIZI**" ina vipengele viwili yaani masomo mawili makuu yanayohusiana na mada husika. Masomo haya yana vipengele vidogo vidogo kama vile: mchoro, kifungu cha habari, maswali ya ufahamu, matumizi ya msamiati, matumizi ya lugha, kusikiliza na kuzungumza na kuandika, sarufi na maelezo muhimu. Somo la kwanza ni "**Dhana ya fasihi simulizi**" na somo la pili lilipewa kichwa cha "**Hadithi**".

## 2.8. Maelezo ya ziada

**Fasihi**

Fasihi ni kazi ya Sanaa inayomulika hisi mawazo na malengo ya jamii kwa kutumia lugha. Fasihi ni sanaa ya lugha inayoshughulikia masuala mbalimbali yanayohusu binadamu. Sanaa ni ufundi wowote wa kuibua mawazo yaliyomo akilini na kuyaonyesha kwa njia mbalimbali. Kila kazi ya sanaa ina wenzo wake kama vinavyoonekana kwenye jedwali lifuatalo:

| **Kazi ya sanaa** | **Wenzo** |
|---|---|
| Fasihi | Lugha (maneno) |
| Ufinyanzi | udongo |
| Sinema | Picha |
| Uchoraji | Rangi |
| Uchongaji | Mti, jiwe |

Fasihi kama kazi ya sanaa inaweza kuelezwa kwa mitazamo miwili. Fasihi ya Kiswahili na Fasihi katika Kiswahili. Fasihi huelimisha, huonya, huelekeza, hukejeli, huhifadhi utamaduni, hukuza lugha. Fasihi huchukuliwa kama kioo cha jamii, mwavuli na hata daraja. Isitoshe, fasihi huchukuliwa kama silaha ya ukombozi

Katika lugha ya Kiswahili kuna aina mbili za fasihi: fasihi andishi na fasihi simulizi. Fasihi andishi ni aina ya fasihi inayohifadhiwa kimaandishi. Fasihi simulizi ni masimulizi ya kale ambayo hayakuandikwa wala kunaswa kwenye vinasasauti. Fasihi simulizi ina vipera vyake kama vile hadithi, nahau, methali, vitendawili, misemo na ushairi.

Katika fasihi simulizi ya Kiswahili kuna hadithi za aina nyingi: hekaya, hurafa, ngano, visasili, visakale, miviga, mighani, na kadhalika.

## 2.9. Tathmini ya mada

1) Fasihi ni kazi ya sanaa inayomulika hisi, mawazo na malengo ya jamii kwa kutumia lugha.
2) Fasihi ina umuhimu katika jamii kwa sababu inaelimisha wanajamii, inawaonya, inawaburudisha, inawaelekeza, inahifadhi utamaduni wao, inalinda utamaduni wao.
3) Hapana! Haiwezekani kutenganisha fasihi na jamii kwa sababu fasihi huchambua jamii. Fasihi haiwezi kuwepo bila jamii.
4) Tunalinganisha fasihi na mwavuli kwa sababu fasihi inalinda utamaduni wa jamii ili usiingiliwe na mambo mengine kutoka tamaduni nyingine.
5) Hadithi ni mambo ya kubuni ambayo huwa yanaeleza ukweli fulani katika jamii.

6) Aina za hadithi: hekaya, hurafa, ngano, mighani, miviga, soga, n.k.

7) Aina za maneno katika sentensi zifuatazo:

i) Yeye ana mkono mrefu, atafungwa.
W t N V T

ii) Nchi yetu ni nchi ya amani.
N V t N V N

iii) Baba alikuwa akiendesha gari.
N TS T N

iv) Wengine warefu wamewasili.
W V T

v) Dawa ya moto ni moto.
N V N t N

## 2.10. Kazi za ziada

### 2.10.1. Kazi za urekebishaji

**Kazi ya 1:** Eleza kwa kina fasihi simulizi

**Jibu:** Fasihi simulizi ni masimulizi ya kale ambayo hayakuandikwa wala kunasiwa kwenya vinasasauti. Hii ni fasihi asilia na kongwe zaidi duniani na ndiyo mzazi wa vipera vyote vya fasihi andishi.

### 2.10.2. Kazi jumuishi

**Kazi ya 2:**

- Taja sifa za fasihi simulizi.

**Majibu:** Hupitishwa kwa njia ya mdomo, masimulizi yake yanaweza kuathiriwa na mazingira, hisia na hali. Fasihi simulizi ni mali ya jamii, n. k.

- Taja methali hamsini za Kiswahili.

**Mwelekeo:** Wanafunzi wapewe kazi ya nyumbani ili kutafuta methali hamsini za Kiswahili na kueleza jinsi zinavyotumiwa.

### 2.10.3. Kazi za nyongeza

**Kazi ya 3:** ***Ni nini umuhimu wa kusoma Fasihi katika Kiswahili kwa mwanafunzi (mambo matano)?***

**Mwelekeo:** - Fasihi inasaidia wanafunzi kukuza lugha kimsamiati

- Fasihi hukuza uwezo wa wanafunzi wa kuzungumza lugha kwa ufasaha

- Fasihi inaweza kuwa chanzo cha kujikomboa kifikra na kiuchumi kwa wanafunzi

- Fasihi inaweza kusaidia wanafunzi kuelewa historia na utamaduni wao, n. k.

# MADA YA 3

# METHALI NA SEMI FUPIFUPI

## 3.1. Uwezo upatikanao katika mada

Kutumia methali na semi fupifupi katika maisha ya kila siku.

## 3.2. Ujuzi wa awali

Somo hili halina ujuzi wa awali kusema kweli, lakini sarufi yake ina ujuzi wa awali katika kidato cha pili kiwango cha kwanza katika shule za upili ambapo mwanafunzi alisoma kuhusu vielezi, vihusishi, vihisishi na viunganishi pamoja na aina nyingine za maneno ya Kiswahili.

## 3.3. Kuingizwa kwa masuala mtambuka katika mada

Katika mada hii ambayo ina somo moja, mkufunzi ataingiza masuala mtambuka katika kufundisha na hata katika kazi zote zitakazofanywa na wanafunzi kama ifuatavyo:

**Mafunzo kuhusu amani na maadili**

Katika kuainisha maneno mbalimbali, sentensi zitakazotumiwa lazima ziwe na mwelekeo wa kuimarisha amani na maadili. Kwa kutunga sentensi, mkufunzi awaongoze wanafunzi kutunga sentensi zenye mafunzo yanayohusu amani na maadili.

**Elimu isiyo na ubaguzi**

Makundi ya wanafunzi wenye mahitaji maalumu ya kielimu kama vile: wanafunzi wenye matatizo kama vile ulemavu wa mwili, wanafunzi wenye kipaji maalumu katika uwezo wa kujifunza, n.k. watasaidiwa kwa upekee ili nao wapate maarifa na maadili yanayotakiwa. Kwa hiyo, ni lazima mkufunzi awasaidie kama vile:

- Kuwaambia wale wenye tatizo la kutoona au kutosikia vizuri wakae kwenye madawati yaliyoko karibu na mkufunzi;
- Kuzingatia matatizo ya kila mwanafunzi, kumtega sikio na kuelewa mahitaji yake;
- Kupanga kazi maalum zilizoandikwa kwenye karatasi kwa wanafunzi wenye matatizo fulani;

- Kuwachanganya na wengine katika makundi mbalimbali wakati wa kufanya kazi kwa pamoja;
- Kutowasimanga na kutowakashifu wanafunzi wenye matatizo mbalimbali kama vile wale wanaotoka katika familia fukara, wale wenye matatizo ya kielimu, wale wasiosema vizuri na kadhalika.

**Usawa wa jinsia**

Katika mojawapo ya mifano ambayo itatolewa darasani, mkufunzi atatumia ile ambayo inaonyesha usawa wa jinsia. Wakati wa kazi za makundi, mkufunzi atapanga wavulana na wasichana kwa pamoja katika kujenga makundi ya kufanyia kazi hizo.

**Mafunzo kuhusu mauaji ya kimbari**

Mkufunzi atahakikisha kwamba methali na nahau zitakazotumiwa, sentensi zihusuzo sarufi na zile za matumizi ya msamiati hazishawishi wanafunzi kujihusisha na itikadi ya mauaji ya kimbari kama vile mauaji ya kimbari dhidi ya Watutsi mnamo mwaka 1994.

## 3.4. Mwongozo kuhusu kidokezo cha mada

Kwa kutangulia mada, mkufunzi aulize maswali ambayo yatawasaidia wanafunzi kufunua mada hii. Wanafunzi wanaweza kushindwa kutoa majibu sahihi mwanzoni, lakini wanaweza kufanikiwa kwa kupitia maswali tofauti ya mazoezi au kazi nyingine zilizotayarishwa mwanzoni mwa mada hii.

Maswali yatakayoulizwa katika kidokezo lazima yawe yanahusiana na masomo husika.

## 3.5. Orodha ya masomo na tathmini

| | Kichwa cha somo | Malengo ya kujifunza (kutoka muhtasari: maarifa na ufahamu, stadi na maadili na mwenendo mwema) | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|
| 1 | **Methali na nahau (semi fupi)** | **Maarifa na ufahamu:**<br>- Kueleza maana ya methali.<br>- Kutoa maelezo ya nahau (semi fupi).<br>- Kuonyesha umuhimu wa methali na nahau (semi fupi) katika jamii.<br>- Kutaja aina za maneno nakueleza matumizi yake.<br>**Stadi:** - Kutumia methali na nahau (semi fupi) katika mazungumzo<br>- Kutambua methali na semi nahau (semi fupi) katika mahojiano na kutetea umuhimu wake katika jamii.<br>- Kutumia kwa usahihi aina za maneno<br>- Kutunga kifungu kuhusu methali<br>**Maadili na mwenendo mwema:**<br>- Kuonyesha adabu na hehima kwa watu anaoongea nao<br>- Kukuza tabia na mwenendo wa kutumia lugha inayofaa kwa heshima yake na ya watu wengine<br>- Kudumisha ushirikiano na watu mbalimbali kupitia mahojiano.<br>- Kutumia methali ambazo zitasaidia kuendeleza umoja na maridhiano katika jamii. | 5 |
| **Tathmini ya mada** | | | 2 |
| **Idadi kamili ya vipindi** | | | 7 |

# SOMO LA 4: METHALI NA NAHAU (SEMI FUPI)

**a) Malengo ya ujifunzaji**

- Kueleza maana ya methali,
- Kutoa maelezo ya nahau (semi fupi),
- Kueleza ujumbe unaopatikana katika methali na semi fupifupi,
- Kuonyesha umuhimu wa methali na nahau (semi fupi) katika jamii,
- Kutumia methali na nahau (semi fupi) katika mazungumzo,
- Kutumia kwa usahihi aina za maneno,
- Kukuza tabia na mwenendo wa kutumia lugha inayofaa kwa heshima yake na ya watu wengine,
- Kudumisha ushirikiano na watu mbalimbali kupitia mahojiano Kuzitumia methali ambazo zitasaidia jamii,

**b) Zana au vifaa vya ufundishaji**

Ili somo liweze kufika kwenye malengo yake, ni lazima mkufunzi ajaribu kutafuta zana za ufundishaji zitakazomsaidia kufanikisha somo lake ili kukidhi mahitaji ya wanafunzi na malengo ya somo husika.

Katika somo hili zana muhimu ni: Kitabu cha mwanafunzi, mwongozo wa mkufunzi, vinasa sauti, Kamusi ya Kiswahili Sanifu, ubao, chaki na vifaa vinavyoweza kuwasaidia wanafunzi kuelewa somo akifuatilia kwa karibu mkazo juu ya hali za wanafunzi wanaohitaji uangalifu maalumu kama wale wenye shida mbalimbali.

**c) Ujuzi wa awali/Marudio/Utangulizi**

Mada hii inajishughulisha na msamiati na majadiliano kuhusu utumiaji wa methali na nahau (semi fupi). Mkufunzi aanze somo kwa kuwaamkia wanafunzi. Nao wajibu maamkizi ya mkufunzi kisha mkufunzi atangulize somo kwa kuwauliza maswali mepesi ya kuwachangamsha. Maswali haya yatakuwa na uhusiano wa karibu na nahau pamoja na methali.

Mkufunzi atakachofanya ni kuwashirikisha wanafunzi wake ili waweze kuwasiliana kuhusu utumiaji wa methali na nahau kisha afanye chochote ili awawezeshe kufika kwenye kile ambacho anadhamiria kufundisha. Baada ya kufanya kazi hii, mkufunzi awaambie wanafunzi kujenga makundi na kutazama mchoro uliomo katika kitabu cha mwanafunzi, kisha awaulize maswali kuhusu mchoro. Mifano ya maswali ni kama ifuatayo:

- Elezea wahusika unaowaona kwenye mchoro.
- Matukio haya yanafanyikia wapi?

- Ni shughuli zipi zinazofanyika kwenye mchoro?

**d) Maelekezo kuhusu kazi za ujifunzaji**

Katika hatua hii, mkufunzi atafute mbinu mbalimbali zitakazomwezesha kufika kwenye malengo ya somo lake. Katika somo hili mkufunzi atilie mkazo mambo yafuatayo:

- **Utumiaji wa makundi ya wanafunzi**: Ni lazima mbinu hii itumiwe ili kumshirikisha mwanafunzi katika mambo yote yanayofanyiwa darasani. Wanafunzi watumie makundi yao kwa kufanya kazi zote watakazopewa na mkufunzi na zile zipatikanazo katika kitabu cha mwanafunzi. Wafanye kazi katika makundi ya idadi mbalimbali za wanafunzi kulingana na ukubwa wa darasa na hali ya kazi.
- **Kazi binafsi kwa mwanafunzi**: Ni lazima kila mwanafunzi apewe kazi yake binafsi. kwa mfano: Kusoma kifungu cha habari, kufanya majaribio, mitihani mbalimbali na hata kazi za nyumbani.
- **Maswali na majibu**: Mara nyingi somo huwa na majadiliano kati ya mkufunzi na wanafunzi. Kuhusiana na mbinu hii, mkufunzi awaulize wanafunzi maswali mbalimbali nao wajibu maswali hayo. Vilevile, nao wamuulize mkufunzi maswali kadhaa naye ayajibu. Tena, maswali na majibu haya yawe kati ya wanafunzi wenyewe.
- **Majadiliano**: Mbinu hii iwawezeshe wanafunzi kujadiliana kuhusu methali na nahau mbalimbali katika kazi mbalimbali watakazopangiwa na mkufunzi.
- **Maelezo ya mkufunzi**: Mbali na kuwa mwanafunzi hupewa kipaumbele katika somo, mkufunzi angali mwezeshaji katika somo lake. Kwa hiyo, atumie mbinu hii kwa kueleza mambo yatakayohitaji maelezo yake ili kufanikisha somo lake.
- **Utafiti**: Mbinu hii inaruhusu wanafunzi kutafuta maelezo zaidi kuhusu kazi watakazopangiwa na mkufunzi. Watafute habari mbalimbali katika vitabu vya maktabani au kwa kutumia tovuti. Wanaweza pia kujadiliana na watu wengine wa nje ya darasa lao.

Katika kufanya kazi mbalimbali, mkufunzi atakuwa na jukumu kubwa la kuwaelekeza wanafunzi hatua kwa hatua, pamoja na kuwasaidia iwezekanavyo kwa minajili ya kuhakikisha kwamba malengo ya masomo yanafikiwa. Yafuatayo ni majibu ya maswali ambayo yanatarajiwa kutolewa na wanafunzi katika somo hili.

**e) Majibu:**

**Kidokezo:** ***Wanafunzi watatazama michoro na kutoa majibu mkufunzi akiwaongoza. Wataelezea watakachoona kwenye mchoro na shughuli ambazo zinaendelea hapo hapo. Yafuatayo ni majibu yaliyopendekezwa:***

Kuna wanaume wawili walio mbele ya mwanamke mmoja akibeba mtoto mikononi. Wanaume hawa wanataka kumchukua mtoto yule. Kuna pia watoto wao wawili wanaosimama nyuma ya wanaume hao.

**Kusoma na ufahamu: Leo ni leo**

**Kazi ya 1:** ***Majibu ni haya yafuatayo:***

1) Mzee Gahigi na mtoto wake Kagabo.
2) Maneno yake yalikuwa yamejaa hekima.
3) Mzee Gahigi alikuwa mpatanishi.
4) Kagabo alianza kuwa na tabia ya uzembe. Lakini kutokana na mawaidha ya baba yake alibadilika akawa mtendakazi.
5) "Mchumia juani hulia kivulini." Methali hii inahusiana na kifungu cha habari nilichosoma kwani Kagabo alitumia nguvu zote alizokuwa nazo alipokuwa akisoma kwa kutayarisha maisha yake yajayo na mwishowe akafanikiwa.
6) Funzo ni kwamba ni vizuri kufanya kanzi tukiwa bado na uwezo bila kungoja kesho. Kagabo anayesimuliwa katika kifungu alifanya kama vile na kufanikiwa baadaye.

**Msamiati kuhusu methali**

**Kazi ya 2:**

1) **Mafumbo:** maneno yasiyojulisha maana waziwazi
2) **Mawaidha:** maneno yenye maonyo au mafunzo, mashauri.
3) **Maktaba:** nyumba au chumba mnamohifadhiwa vitabu ambamo watu huruhusiwa kuvisoma au kuviazima kwa muda.
4) **Shaka:** hali ya kutokuwa na hakika ya jambo; wasiwasi, tuhuma, hatihati, wahaka.
5) **Baraka:** mambo mema kwa jumla; mafanikio, fanaka, neema, heri.

**Kazi ya 3:**

1) **Leo ni leo asemaye kesho ni mwongo:** Jambo linalowezekana kutendwa sasa hivi, lazima litendwe bila kuahirishwa.

2) **Chelewa chelewa utamkuta mtoto si wako:** Ukisubiri kutenda jambo kama likiwa likiwezekana hutapata manufaa yake.

3) **Ndege aamkaye asubuhi hula wadudu watamu:** Mtu anayeamka mapema na kutenda kazi ndiye anayefanikiwa.

4) **Wakati titi la nyati hukamuliwa kwa mashaka:** Chunga wakati unaokuwa nao na kuutumia vilivyo, unaweza kukuacha bila kufanya ulichotarajia kufanya.

5) **Haraka haraka haina baraka:** Usifanye mambo kwa pupa.

6) **Ngoja ngoja huumiza matumbo:** Kusubiri jambo fulani kwa muda mrefu kunasumbua.

7) **Wakati una mabawa:** Wakati unakimbia sana.

8) **Mchumia juani hulia kivulini:** Mtu anayefanya kazi ngumu ikiwepo hata katika mazingira ya jua huja kufaidi matunda ya kazi ngumu akiwa amestarehe.

**Sarufi kuhusu matumizi ya vielezi, viunganishi, vihusishi na vihisishi**

**Kazi ya 4:**

1) **Sawasawa:** Kielezi cha namna.

2) **Kitoto:** Kielezi cha namna

   **Kwelikweli:** Kielezi cha namna

3) **Kwa:** Kielezi cha namna

   **Lilelile:** Kielezi kisisitizi

4) **Lelelele lelelele:** Kielezi cha namna

   **Juzi:** Kielezi cha wakati.

5) **Polepole:** Kielezi cha namna

**Kazi ya 5:**

1) Hana nyuma **wala/au/ama/na** mbele.

2) Musabyimana alikula staftahi **kisha/pia/tena** aliendа ofisini.

3) Alimsogelea adui yake **lakini/tena/pia** hakuwa na hofu.

**Kazi ya 6:** ***Tunga sentensi ukitumia viunganishi vinavyofuata:***

1) Mbali na: Kigali ni **mbali na** Butare.

2) Baada ya: **Baada ya** kazi nitaenda kanisani kusali.

3) Lakini: Ninapenda chakula sana **lakini** sipendi kukimbia.

**Kazi ya 7:**

1) Kitabu hiki ni **Sawa na** kile.
2) Alikimbizwa hadi **karibu na** nyumba yake.
3) **Baada ya** kula chakula tulinawa mikono.
4) Walisoma **hadi** usiku wa manane.
5) Alienda **moja kwa moja** kwa mwalimu mkuu.

**Kazi ya 8:**

1) **Haki ya Mungu!:** Kihisishi.
2) **oyee!:** Kihisishi.
3) **Ala!:** Kihisishi.
4) **Afanaalek!:** Kihisishi.
5) **Huree!:** Kihisishi.

**Matumizi ya lugha: Methali na nahau (semi fupi)**

**Kazi ya 9:** ***Mkufunzi awasaidie wanafunzi kujenga makundi ya watatu watatu au wanne wanne, awashirikishe kusoma maelezo muhimu, kisha wajibu maswali.***

1) Methali ni tungo fupi za sentensi moja ambazo hutoa funzo fulani kwa njia ya mafumbo.
2) **Mifano ya methali**

   Chelewa chelewa, utamkuta mtoto si wako.

   (Hoja) (Matokeo)

   Wakati titi la nyati, hukamuliwa kwa shaka.

   (Hoja) (Suluhisho)

**3. Mifano ya methali:**

**a) Mpanda ngazi hushuka**

- **Maana ya nje:** *Mtu yeyote anayepanda juu ya ngazi ni lazima itafika muda wake kushuka kutoka juu ya ngazi hiyo.*
- **Maana ya ndani:** *Katika maisha mtu anayepata cheo au madaraka kuna siku anaweza kuyapoteza madaraka au cheo hicho.*

**b) Leo ni leo asemaye kesho ni mwongo**

- **Maana ya nje:** *Siku hii ni siku hii, anayenena siku ifuatayo ni mdanganyifu.*
- **Maana ya ndani:** *Tendo linalowezekana kufanyika sasa lazima lifanyike, lisiahirishwe.*

**Kazi ya 10: *Husisha methali kutoka orodha ya A na methali yenye maana sawa katika orodha ya B***

**Majibu ya swali la 10:** 1 (g), 2 (i), 3 (a), 4 (b), 5 (h), 6 (c), 7 (f), 8 (j), 9 (d), 10 (e)

**Kazi ya 11: *Linganisha methali za sehemu A na maana mwafaka kutoka katika sehemu B.***

**Jibu la swali la 11:** 1 (e), 2 (d), 3 (b), 4 (a), 5 (c).

**Kazi ya 12: *Tumia mshale kwa kuhusisha nahau katika sehemu A na maana zake katika sehemu B.***

**Majibu:** 1 (e); 2 (d) ; 3 (f); 4 (g); 5 (b); 6 (j); 7 (c); 8 (h); 9 (i); 10 (a).

**Kazi ya 13:**

***Majibu:*** *Nahau na maana sawa*

| **Sehemu A** | **Sehemu B** |
|---|---|
| 1. Kushika hatamu | A. Kuongoza |
| 2. Kula unga | B. Kupata kazi |
| 3. Kushika miguu | C. Kutoa shukrani / kuomba radhi |
| 4. Kukata kamba / kuaga dunia | D. Kufariki |
| 5. Kumpa nyama ya ulimi | E. Kudanganya mtu na maneno matamu |
| 6. Kumeza maneno | F. Kutunza siri moyoni |
| 7. Kula njama | G. Kufanya mkutano wa siri |
| 8. Kupiga uvuvi | H. Kukaa tu bila kazi |
| 9. Kuoga mwaka | I. Kusherehekea kumaliza mwaka kwa salama |
| 10. Kupiga ubwana | J. Kukaa bila kufanya kazi wakati wa kazi |

**Kusikiliza na kuzungumza: Majadiliano**

**Kazi ya 14:** ***Katika makundi ya wanafunzi wawili, wajadiliane kuhusu maana na matumzi ya nahau zifuatazo:***

1) **Kuchemsha bongo:** Kufikiri sana
2) **Kuchongea mtu:** kusingizia mtu makosa
3) **Kubeza mtu:** Kudharau mtu
4) **Kuchungulia kaburi:** Kuumwa na kukaribia kufa
5) **Kufafanua kinaga-ubaga:** Kufafanua kwa undani
6) **Kupigwa kalamu:** Kufukuzwa kazini
7) **Kumpa nyama ya ulimi:** Kumpa mtu maneno matamo

**Kuandika: Utungaji wa insha ya methali**

**Kazi ya 15: Mwanafunzi atatunga kifungu cha habari chenye mada ifuatayo***:* *"Mchumia juani hulia kivulini."* ***Atahakikisha kwamba anatumia vielezi, viunganishi, vihusishi, vihisishi na baadhi ya nahau mojawapo ya hizi ambazo zinafuata:***

**Kufunga virago:** kuondoka; kusafiri

**Kugaragara kitandani:** kugeukageuka kitandani

**Kujifungua mtoto:** kuzaa kwa mwanamke

**Kukata kamba:** kufariki

**Kukaza kamba:** kujitahidi

**Kula chumvi nyingi:** kuishi miaka mingi

**Kula kiapo:** kuapa

**Kumpa mtu heko:** kupongeza mtu

**Kumpa mtu mgongo/kisogo:** kufanyia mtu mambo yaliyo kinyume na matarajio

**Kumpa mtu nyama ya ulimi:** kumpa mtu maneno matamu

**Kuona cha mtemakuni:** kujuta; kupata adhabu kali

**Kuona kilichomnyima nyoka miguu:** kupata adhabu kali.

**Kuona kilichomnyima kanga manyoya:** kupatwa na ubaya.

**Kupanda mbegu za chuki:** kuchochea watu wachukiane

**Kupiga marufuku:** kukataza kitu kisheria

**Kuvunja mbavu:** kuchekesha; kufanya au kusema maneno yanayochekesha.

**Kuvunja nyumba:** kuharibu hali ya maisha baina ya mume na mke.

## 3.6. Kazi ya utafiti

Wanafunzi wapewe kazi ya utafiti kuhusu matumizi ya methali na umuhimu wake katika jamii. Kila mwanafunzi aeleze angalau methali tano.

## 3.7. Muhtasari wa mada

Mada hii ya tatu **"Methali na semi fupifupi"** ina somo moja. Somo hili lina vipengele vidogo kama vile: mchoro, kifungu cha habari, maswali ya ufahamu, matumizi ya msamiati, sarufi, matumizi ya lugha, kusikiliza na kuzungumza, kuandika, pamoja na na maelezo muhimu. Ndani ya somo hili, kuna maana ya methali na nahau pamoja na umuhimu wake katika jamii. Kuna maelezo na matumizi ya kutosha kuhusu aina za maneno kama vile vielezi, vihusishi, vihisishi na viunganishi. Mwisho wake, kuna tathmini ya mada kwa ujumla.

## 3.8. Maelezo ya ziada kwa mkufunzi

Sehemu hii inahusu maelezo ya ziada kwa mkufunzi. Katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji, inambidi mkufunzi kuwa mbunifu na mgunduzi. Hii ni kusema kuwa ana uhuru wa kutafuta mifano mingine ya methali au nahau nyingine na kuzitumia katika ufundishaji wake.

## 3.9. Tathmini ya mada

Mkufunzi awaongoze wanafunzi kujibu maswali ya tathmini na kuchunguza kuwa mambo muhimu yanayozingatiwa na maswali yanapatikana katika majibu ya wanafunzi.

1) **Methali** ni tungo fupi za sentensi moja ambazo hutoa funzo fulani kwa njia ya mafumbo. Ni tamko lenye kueleza wazo la busara la binadamu kwa ufupi sana.

2) **Nahau** ni semi zinazotofautiana na maana yake ya nje. Huwa ni semi zenye mvuto na utamu wa lugha. Nahau huundwa kwa lugha ya kawaida, kwa kuashiria wazo la picha kutoka katika hali halisi ya maisha, ambazo aghalabu huwa ni misemo ambayo mtumiaji huitumia katika maazungumzo au maandishi bila kujua kuwa anaitumia.

3) Umuhimu wa methali ni kuonya, kutoa mafunzo, kutahadhalisha na kuunganisha jamii.

4) Aina za maneno ambayo yamepigiwa misitari katika sentensi zifuatazo:

   a) Kesho: Kielezi cha wakati.

b) Mbele ya: Kihusishi.

c) Chini ya: Kihusishi.

d) Oyeee!: Kihisishi.

e) Na: Kiunganishi.

5) Kila mwanafunzi atajadili kuhusu mada hii "Mtoto umleavyo ndivyo akuavyo."

kwa kutozidi ukurasa mmoja ambapo mkufunzi ataomba wanafunzi kusomea majadiliano yao hadharani baada ya kuyatungia kwenye karatasi zao binafsi kwa kuandika.

## 3.10. Kazi za ziada

### 3.10.1. Kazi za urekebishaji

***Mapendekezo ya maswali na majibu ya kuwasaidia wanafunzi wenye kipaji cha hali ya chini.***

***1) Eleza nahau zifuatazo:***

a) Kupigwa kalamu

b) Kumpa nyama ya ulimi

**Majibu:** a) Kufutwa kazini

b) Kumpa mtu maneno matamu

***2) Tumia vihusishi vifuatavyo kukamilisha sentensi: Sawa na, karibu na, baada ya, hadi, moja kwa moja.***

a) Kitabu hiki ni ……………………………….. kile.

b) Alikimbizwa hadi …………………………….. nyumba yake.

c) ………………………………... kula chakula tulinawa mikono.

d) Walisoma ………………………….. usiku wa manane.

e) Aliendа …………………………… kwa mwalimu mkuu.

**Majibu:** a) sawa na

b) karibu na

c) baada ya

d) hadi

e) moja kwa moja

### 3.10.2. Kazi jumuishi

***Tunga sentensi mbili kwa kila swali yaani sentensi kumi (10) kwa ujumla, ukitumia viunganishi, vihusishi, vielezi na vihisishi vinavyofuata:***

1) Kumbe!

2) Haraka
3) Nyuma ya
4) Hadi
5) Katika

**Majibu:**

1) Nilidhani wewe ni rafiki yangu. Kumbe!

2) Kimbieni haraka ili msichelewe!

3) Kamali anasimama nyuma ya darasa letu.

4) Nimesoma kitabu hiki toka asubuhi hadi sasa.

5) Mwalimu ametufundisha jinsi ya kuweka sentensi kanushi katika hali yakinishi.

### 3.10.3. Kazi za nyongeza:

Mapendekezo ya maswali na majibu kwa wanafunzi wenye kipaji cha hali ya juu cha werevu.

**Maswali**

1) Jadili kwenye kurasa mbili mada hii "Mtoto umleavyo ndivyo akuavyo."
2) Ni methali ipi inayoweza kutumiwa wakati mtu fulani ameshindwa kutimiza aliyoyasema?

**Mwelekeo:**

1) Mkufunzi akumbushe wanafunzi jinsi ya kufafanua methali wakizingatia maana ya ndani ya methali na maana yake ya nje. Awakumbushe pia sehemu kuu za insha kama vile: Anwani, utangalizi, muwili na hitimisho.

2) Ahadi ni deni.

# MADA YA 4

# MJADALA

## 4.1. Uwezo Mahususi upatikanao katika mada

Kusikiliza kwa makini maoni ya washiriki wa mjadala na kutoa hoja binafsi.

## 4.2. Ujuzi wa awali

Kupitia masomo waliyofundishwa katika kidato cha tatu, mada kuu: "Ukuzaji wa lugha kimazungumzo" ilizungumzia masomo tofauti kama vile: "Midahalo na mijadala." Wanafunzi hawa wana ujuzi wa jumla kuhusu msamiati wa "Mjadala." Vilevile, wanafunzi hawa wana ujuzi kuhusu "maandalizi na utekelezaji wa mjadala.’’

## 4.3. Kuingizwa kwa masuala mtambuka katika mada

Katika masomo ya mada hii kwenye vifungu, michoro au picha, utumiaji wa msamiati katika sentensi, matumizi ya lugha na katika mazoezi au kazi na sarufi; mkufunzi atawaongoza wanafunzi katika ujifunzaji na kutumia masuala mtambuka yafuatayo:

- **Mafunzo kuhusu uzalishajimali/ujasiriamali**
  Katika masomo ya mada hii kwenye vifungu, utumiaji wa msamiati, katika sentensi; mkufunzi atawaongoza wanafunzi kwenye mjadala. Hapa, mkufunzi atawaongoza wanafunzi na kuwaonyesha kuwa kuandaa mjadala na kuzungumza hadharani ni mojawapo ya njia mwafaka ya kujiendeleza katika fani ya lugha kwa kubainisha mwongozo wa kuongoza mjadala. Ujuzi wa kuandaa na kuongoza mjadala unaweza kuwasaidia wanafunzi kujipatia ajira katika shughuli tofauti zinazohusisha maandalizi na utekelezaji wa mjadala.

- **Mafunzo kuhusu amani na maadili**
  Wanafunzi watumie msamiati unaoimarisha amani na maadili katika majidiliano yao. Mkufunzi aeleze wanafunzi kuwa ingawa wanaweza kuwa na hoja tofauti lakini lazima ziwe zinajenga jamii.

- **Elimu Jumuishi**

  Makundi ya wanafunzi wenye mahitaji maalumu ya kielimu kama vile: Wanafunzi wenye matatizo ya ulemavu /ulemavu wa mwili, wanafunzi wenye kipaji maalumu katika uwezo wa kujifunza, n.k. washughulikiwe vilivyo.

  Mkufunzi anapaswa kukumbuka kuwa wanafunzi wenye matatizo kama haya ni kama wengine; walikuja shuleni ili wapate maarifa na maadili yanayotakiwa. Kwa hiyo, ni lazima mkufunzi awasaidie ipasavyo. Kama vile:

  - Kuwaambia wale wenye tatizo la kutoona au kutosikia vizuri wakae kwenye madawati yaliyoko sehemu za mbele karibu na mkufunzi;
  - Kuzingatia matatizo ya kila mwanafunzi, kumtega sikio na kuelewa mahitaji yake;
  - Kupanga kazi maalum zilizoandikwa kwenye karatasi kwa wanafunzi wenye matatizo ya kusikia;
  - Kuwachanganya na wengine katika makundi mbalimbali wanafunzi wenye matatizo ya kuongea na kuwasiliana na wengine, kupewa muda wa kuongea;
  - Kuunda makundi ya wanafunzi kutokana na ujuzi na uwezo wao katika kujifunza;
  - Kupanga kazi au mazoezi kutokana na makundi ya wanafunzi wenye matatizo maalum ya kielimu;
  - Kuwachanganya na wengine katika makundi mbalimbali wanafunzi wenye matatizo ya kimwenendo na kuwachunga ipasavyo;
  - Kuwasiliana na wazazi wa wanafunzi wenye matatizo maalumu ili kusaidiana katika kupata suluhisho kwa matatizo yao;
  - Kushirikiana na viongozi wa shule na wazazi katika kuweka mikakati thabiti ili lugha ya kufundishia isije ikawa kizuizi kwa masomo yao;
  - Kutowasimanga na kutowakashifu wanafunzi wenye matatizo mbalimbali kama vile wale wanaotoka katika familia fukara, wale wenye matatizo ya kielimu, wale wasiosema vizuri na kadhalika;
  - Kuwa mwenye wingi wa huruma na kujua kwamba ulemavu wao au matatizo yao yanajitokeza kwa ghafla na hayatokani na utashi wao au matendo yao, n. k.

- **Mazingira na maendeleo endelevu**

  Mkufunzi kupitia michoro, vifungu, mazoezi ya msamiati na sarufi, anaweza kueleza umuhimu wa kuhifadhi mazingira kwa maisha ya watu. Katika mada hii, anaweza kuandaa mada ambazo huzungumzia kuhusu uhifadhi wa mazingira.

Aidha, mkufunzi anaweza kutoa kazi zinazoeleza madhala ya kuharibu mazingila ili waonyeshe mchango wao katika kuyatunza.

- **Mafunzo kuhusu mauaji ya kimbari/kuangamiza**

  Mkufunzi atazungumzia kuhusu mauaji ya kimbari dhidi ya watutsi na athari zake kwa kupitia kazi tofauti za vifungu vya habari na kazi nyingine za utafiti katika kuelezea suala hili.

## 4.4. Mwongozo kuhusu kidokezo cha mada

- Mkufunzi atoe mwongozo wa kutoa jibu kwa kazi zinazohusu kidokezo.
- Mkufunzi anaweza kuuliza swali kama kuna yeyote anayefahamu kuhusu neno mjadala?
- Anaweza kuwaweka wanafunzi katika makundi ya wanafunzi wawili wawili kisha akapokea majibu ya baadhi ya makundi kulingana na muda wa kipindi ili aweze kuwaelekeza kabla ya kipindi kwisha.
- Mkufunzi anashauliwa kuuliza maswali yanayohusiana na somo litakaloshughulikiwa katika mada hii.

## 4.5. Orodha ya masomo

| | Kichwa cha somo | Malengo ya kujifunza (Maarifa na ufahamu, stadi na maadili na mwenendo mwema) | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|
| 1 | **Mjadala** | **Maarifa na ufahamu:**<br>Kutoa maana ya mjadala<br>**Stadi:**<br>Kuandaa na kuongoza mjadala<br>**Maadili na mwenendo mwema:**<br>Kutumia maneno yenye adabu na heshima wakati wa mjadala. | 4 |
| 2 | **Maandalizi na utekelezaji wa mjadala"** | **Maarifa na ufahamu:**<br>Kubainisha sifa za mjadala<br>**Stadi :**<br>Kutoa ripoti ya matokeo ya mjadala<br>**Maadili na mwenendo mwema:**<br>Kuheshimu hoja au maoni ya wenzake wakati wa mjadala | 2 |
| **Tathmini ya mada** | | | 2 |
| **Vipindi vyote vya mada ya kwanza** | | | 8 |

# SOMO LA 5: MJADALA

**a) Malengo ya ujifunzaji**

- Kutoa maana ya mjadala
- Kubainisha sifa za mjadala
- Kuandaa na kuongoza mjadala
- Kutunga sentensi kwa kutumia viambishi rejeshi

**b) Zana au vifaa vya ufundishaji**

Vifaa vitakavyosaidia mkufunzi ni kama:

- Kitabu cha mwongozo wa mkufunzi,
- Kitabu cha mwanafunzi,
- Magazeti mbalimbali,
- Ubao,
- Chaki,
- Kamusi ya Kiswahili Sanifu,

Mkufunzi anaweza kuandaa vifaa kadhaa viwezavyo kumsaidia kufanikisha somo lake akitilia mkazo kwa wale wanafunzi ambao wana ulemavu fulani. Hapa mkufunzi awe mbunifu wa vifaa au zana za ufundishaji na ujifunzaji.

**c) Ujuzi wa awali/ Marudio/ Utangulizi**

Somo hili linajishughulisha na "Mjadala" ambapo huzungumzia sifa za mjadala. Wanafunzi hawa walisoma katika kidato cha tatu masomo ya: "**Ukuzaji wa lugha kimazungumzo"** katika kitabu cha mwanafunzi kidato cha tatu; kwa hiyo somo hili si jipya kwao. Mkufunzi aulize wanafunzi mmoja mmoja maswali tofauti kuhusu somo lililotangulia kwa kuchunguza ikiwa wanalikumbuka au wana maswali kuhusu somo hilo. Akiona kuwa hawana tatizo aanze somo jipya. Akiona wana matatizo kuhusu somo hilo, ayatatue kabla ya kuanza somo jipya.

**d) Maelekezo kuhusu kazi za ujifunzaji**

Katika hatua hii, mkufunzi atatafuta mbinu mbalimbali zitakazomwezesha kufika kwenye malengo ya somo lake hivi akitilia mkazo mbinu zifuatazo: kazi za makundi, fikiri-jozi-changia, mbinu ya bungua bongo, kazi ya utafiti, n.k.

Mkufunzi ataunda makundi ya wanafunzi kulingana na idadi ya vitabu vilivyoko.

**e) Majibu:**

**Kidokezo :**
*Kidokezo hiki kifanyiwe katika makundi, wanafunzi waweze kujadili maswali na baadaye waeleze wanayoyajua kuhusu mchoro husika.* Yafuatayo ni majibu yaliyopendekezwa:

1) Ninaona watu wanaokaa ukumbini wakisikiliza viongozi wao.
2) Watu hawa wanafanya mjadala.
3) Ni mazungumzo ambayo hufanywa kuhusu suala fulani linalohitaji kujadiliwa na kutafutiwa ufumbuzi.
4) Ni mmoja ambaye ni kiongozi wa mjadala.

**Kusoma na ufahamu: Maana ya mjadala**

**Kazi ya 1:** ***Kusoma kwa kimya kifungu cha habari kuhusu "Mjadala" huku wakiandika msamiati mpya wanaokutana nao kutawasaidia kuelewa zaidi somo hili wakielekezwa na mkufunzi.***

***Mkufunzi aandike kichwa cha somo ubaoni, pamoja na malengo mahususi ya somo husika.***

***Hatimaye, mkufunzi awaulize maswali mbalimbali kuhusu kifungu walichosoma kuhakikisha kuwa wamekielewa. Baada ya kuhakikisha kwamba wanafunzi wamesoma kwa kimya na kuelewa, mkufunzi awaombe wanafunzi mmoja baada ya mwingine kusoma kwa sauti inayosikika kifungu kilichopo. Mkufunzi aongoze wanafunzi kuelezea maana ya maneno mapya yaliyomo kifunguni. Halafu, mkufunzi awaongoze wanafunzi katika makundi yao wafanye kazi zinapatikanazo katika kitabu cha mwanafunzi na mkufunzi atoe msaada kunapohitajika. Mkufunzi asahihishe kazi za wanafunzi katika makundi yao kisha awaongoze katika kufanya masahihisho ya kazi waliyopewa.***

***Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, wasome kifungu cha habari kwa ufasaha na kujibu maswali ya ufahamu. Mkufunzi arekebishe makosa yanayojitokeza katika majibu ya wanafunzi.***

***Majibu yaliyopendekezwa:***

1) Mjadala ni mazungumzo juu ya jambo maalum ambayo hufanywa na watu kwa kutoa hoja zao kwa jambo fulani linalotakiwa ufafanuzi au ufumbuzi wa suala lililopo. Mjadala huhusisha watu wengi wanaotoa hoja kuhusu mada fulani.
2) Katika mjadala, kiongozi ana kazi ya kuongoza majadiliano kwa kupanga muda wa kuzungumza kwa kila msemaji anayeshiriki katika

mazungumzo. Kutokana na hayo, hakuna msemaji ambaye anaruhusiwa kutoa hoja bila kumuomba fursa kiongozi wa majadiliano. Kama kuna wasemaji ambao wanataka kukiuka mada katika hoja zao, kiongozi wa mjadala huwarekebisha kwa kuwakumbusha mada inayotolewa hoja.

3) Ni kwa sababu, kila mshiriki huwa na lengo la kutoa mawazo kwa nia ya kutatua tatizo fulani linalofafanuliwa na kujadiliwa kwa pamoja ili kutafuta ufumbuzi au suluhisho linalofaa.

**Msamiati kuhusu Maana ya Mjadala**

**Kazi ya 2:** ***Mkufunzi amwombe mwanafunzi kufanya zoezi hili kibinafsi. Mwanafunzi atumie kamusi kwa kuelewa maana ya msamiati mpya na kuutumia katika sentensi. Mkufunzi achunguze kazi zinazofanywa na wanafunzi. Achague sampuli ya wanafunzi watatu wawasilishe kazi yao mbele ya darasa. Mkufunzi arekebishe makosa yanayoweza kujitokeza. Mwanafunzi anaweza kutunga sentensi kama zifuatazo:***

1) Wananchi walijadiliana kuhusu suala fulani linalozorotesha maendeleo yao.
2) Hadhira ilikubaliana kuhusu maendeleo ya shirika lao.
3) Wanafunzi walijichagulia wenyewe kiongozi wa darasa.
4) Majadiliano ni nyenzo muhimu ya kutatua migogoro katika jamii.
5) Binadamu hawezi kuishi bila kukumbwa na migogoro.
6) Ni jukumu la kila mmoja wetu kufanya kazi kwa bidii.

**Kazi ya 3:** ***Wanafunzi wajaze nafasi tupu kwa kutumia neno linalofaa kutokana na kifungu walichokisoma. Mkufunzi awasaidie wanafunzi kwa kuwaelekeza.***

1) kipaji
2) kiongozi
3) hadhira
4) kupanga
5) mahojiano
6) mjadala
7) mazungumzo
8) hoja
9) fursa
10) kuwashirikisha

**Sarufi: Matumizi ya viambishi rejeshi kulingana na ngeli za majina**

**Kazi ya 3:**

Jaza nafasi. Tumia 'o' rejeshi iliyo mwafaka

**Kwa mfano:** Wageni wasafirio wameondoka na mizigo yao

1) Viatu **viuzwavyo** ni mitumba.
2) Safari **ziandaliwazo** zinatufurahisha.

3) Wateja **wanunuao** wana pesa kama mchanga.
4) Mikate **iokwayo** itamalizwa yote.
5) Watalii **wafikao** hawatatamani kuondoka.
6) Miche **ipaliliwayo** itanawiri vizuri.

**Matumizi ya Lugha kuhusu Maana ya Mjadala**

**Kazi ya 4:**

1) Si kweli. Mjadala unaongozwa na mtu mmoja au watu wawili ambao wanazusha mawazo na kuhakikisha ikiwa kuna mwenendo mwema kati ya washiriki wa mjadala huo.
2) Kiongozi wa mjadala ndiye anayetoa muhtasari wa mawazo yaliyotolewa.
3) Malengo ya mjadala mzuri:
   - Kukuza uwezo wa kitaaluma na hali ya udadisi kwa washiriki wa mjadala.
   - Kukuza uwezo wa kushawishi watu hadharani ili wakubaliane na mawazo ya msemaji kuhusu jambo fulani.
   - Kumwezesha mtu kupanga mawazo yake kwa mfuatano mzuri wakati anapoandika insha au habari.
   - Kumwezesha mtu kutambua kipaji alicho nacho cha kuzungumza bila aibu mbele ya hadhira.
   - Kukuza stadi ya utumiaji wa lugha kwa kutumia msamiati na matamshi bora ya lugha.
   - Kumzoeza mtu kusikiliza na kupinga au kutetea maoni na hoja za wengine.
   - Kuwapa watu wasaa wa kuelewana na wengine kutoka maeneo mbalimbali.

   Wanafunzi wajadili malengo matatu katikati ya haya yaliyotolewa. Mkufunzi asahihishe kazi zao na kuwaelekeza ipasavyo..
4) Katika mjadala hakuna mshindi kwa sababu kila hadhira hutoa mchango wake kuhusu swala linalojadiliwa. Kila yeyote aliye na hoja huomba fursa ya kuzungumza. Mjadala si mashindano bali lengo la kila msemaji ni kutoa mawazo kwa nia ya kutatua tatizo fulani linalofafanuliwa na kujadiliwa kwa pamoja ili kutafuta ufumbuzi na suluhisho linalofaa na kupata namna bora ya kutenda mambo yanayozungumziwa. Kwa hiyo, hakuna kuwania ushindi; yeyote ambaye ana la kusema huruhusiwa na hutoa hoja kama apendavyo kuhusu mada inayohusika bila kukiuka ukweli uliopo.

5) Wahusika katika mjadala ni kiongozi ambaye ana jukumu la kuongoza majadiliano kwa kupanga muda wa kuzungumza kwa kila msemaji anayeshiriki katika mazungumzo. Hakuna msemaji anayeruhusiwa kutoa hoja bila kumuomba fursa kiongozi wa majadiliano. Pia, kiongozi huwarekebisha kwa kuwakumbusha mada inayotolewa hoja.

   Hadhira hushiriki katika mazungumzo kwa kusikiliza na kutoa mchango wao kuhusu suala linalojadiliwa. Kila yeyote aliye na hoja huomba fursa ya kuzungumza.

**Kusikiliza na Kuzungumza**

**Kazi ya 5:** ***Kazi hii ifanyike katika makundi ya wanafunzi watano watano. Watajadili mada waliyopewa na kila kundi liwasilishe kazi yao. Mkufunzi arekebishe makosa ya kimazungumzo yatakayojitokeza. Mkufunzi ahakikishe kwamba amewashirikisha wanafunzi wote.***

**Mada ni hii ifuatayo:**
"Maendeleo nchini huyafanya maisha ya Wanyarwanda yabadilike kwa kiwango cha juu."

**Kuandika: Utungaji**

**Kazi ya 6:** ***Kazi hii ifanywe kibinafsi. Mkufunzi awaombe wanafunzi kila mmoja kutoa wasilisho lake mbele ya darasa, kuhusu ubaya wa dawa za kulevya kisha ayaweke pamoja mawazo waliyoyatoa ili kuunda majibu sahihi.***

# SOMO LA 6: MAANDALIZI NA UTEKELEZAJI WA MJADALA

**a) Malengo ya ujifunzaji**

- Kuandaa na kuongoza mjadala
- Kutoa ripoti ya matokeo ya mjadala
- Kujenga ushirikiano
- Kutumia viambishi rejeshi kulingana na ngeli za majina

**b) Zana au vifaa vya ufundishaji na watu wengine**

Vifaa vitakavyosaidia mkufunzi ni hivi vifuatavyo:

- Kitabu cha mkufunzi
- Kitabu cha mwanafunzi
- Kamusi ya Kiswahili Sanifu
- Ubao
- Chaki

Mkufunzi anaweza kuandaa vifaa vingine vinavyoweza kusaidia wanafunzi wenye ulemavu mbalimbali.

**c) Ujuzi wa awali/Marudio/Utangulizi**

Somo hili lina uhusiano na somo la tano lililotangulia. Kwa hiyo, mkufunzi atangulize somo hili kwa kufanya marudio kuhusu somo la kipindi kilichopita. Hii itamsaidia kuchunguza ikiwa wanafunzi wana vikwazo fulani kuhusu somo hilo ili aweze kuwasaidia kabla ya kufundisha somo jipya.

**d) Maelekezo kuhusu kazi za ujifunzaji**

Katika somo hili, mkufunzi atumie mbinu zifutazo:

- Kazi za makundi: Hii itasaidia wanafunzi kushirikiana na kujadiliana ili kufikia jibu sahihi.
- Kazi binafsi: Hii itasaidia kujenga tabia ya kujitegemea kwa mwanafunzi. Kazi hizi zinaweza kuhusisha kusoma kifungu cha habari, majaribio, mitihani, n.k.

**e) Majibu ya kazi zilizotolewa**

Kazi zilizotolewa katika kitabu cha mwanafunzi zina mapendekezo ya majibu katika mwongozo huu. Yafuatayo ni majibu yaliyopendekezwa:

**Kazi ya 1 :**
a) Mjadala ni mazungumzo juu ya jambo fulani linalohitaji suluhisho.

b) Ni kiongozi na hadhila yake (washiriki)

c) Kiongozi huongoza mjadala, hutoa fursa kwa washiriki ya kuzungumza, n. k. wakati ambapo hadhira huchangia ili kutoa hoja zinazolenga kutoa suluhisho.

**Kusoma na ufahamu: Mjadala kuhusu "Mchango wa wazazi katika malezi ya watoto wao"**

**Kazi ya 2:** ***Wanafunzi wajibu maswali ya ufahamu katika makundi ya wanafunzi watatu watatu wakiongozwa na mkufunzi. Mkufunzi atathmini kazi za wanafunzi. Yafuatayo ni majibu:***

1) Malezi ya msingi, mtoto huyapata kutoka kwa wazazi wake nyumbani. Nyumbani ndipo mtoto anapopata malezi ya msingi ambayo humumulikia na humsaidia kufanikiwa katika maisha yake.

2) Dawa za kulevya husababisha magonjwa mengi na huharibu ubongo wa watoto.

3) Mzazi ana wajibu wa kuwapeleka watoto shuleni kwa sababu ndipo mtoto anapata mwenendo mwema utakaomsaidia maishani mwake.

4) Taifa lilirahisisha watoto wote kusoma ilipochukua uamuzi wa kuanzisha mradi wa elimu kwa wote ambapo kila mtoto anapelekwa shuleni akaendelea na masomo yake mpaka anapomaliza shule za sekondari bila malipo yoyote.

5) Viongozi na walimu hutakiwa kuwapatia watoto maadili mema, kuwaelimisha na kuwasaidia katika urekebishaji wa mienendo mibaya.

6) "Mtoto hutazama kisogo cha mama yake". Msemo huu humaanisha kuwa mzazi ni mfano unaoigwa na mtoto wake. Kwa hiyo, mzazi akiwa na tabia nzuri mtoto naye bila shaka ataathiriwa vizuri na itakuwa kinyume kama mzazi ana tabia zisizopendeza. Kwa maneno mengine watoto huiga tabia za wazazi wao.

7) Mtu haulizwi kitu asichokuwa nacho. Tabia ambayo unayo ndiyo utakayoonyesha watakaokutembelea huwezi kuonyesha tabia nyingine ambayo hauna. Mtu ambaye anafanya kazi yake vizuri hupata zawadi yake na matukio mema kutokana na namna alivyofanya kazi yake.

   Ukitaka kufanikiwa lazima ujishughulishe. Watu wenye tabia mbaya huzaa mtoto mwenye tabia mbaya pia. Ukifuata mtu mwenye tabia mbaya bila shaka utakuwa na tabia mbaya na ukifuata mtu mwenye tabia nzuri bila shaka utakuwa na tabia nzuri.

8) Masomo kutoka mjadala ni haya yafuatayo: kulinda watoto kutumia dawa za kulevya, kuwapeleka watoto shuleni na kufuatilia masomo na mienendo yao kokote wanakoenda, kushirikiana na viongozi wa shule pamoja na walimu katika kuendeleza malezi ya watoto na ninaelewa kwamba kila mtu anaweza kumwathiri mtoto vizuri au vibaya.

**Msamiati kuhusu andalio la mjadala**

**Kazi ya 3:** ***Zoezi hili ni la binafsi, mkufunzi awaombe wanafunzi kutunga sentensi kwa kutumia msamiati waliopewa katika sentensi yenye maana. Baada ya hayo awaongoze wanafunzi kufanya masahihisho ya maswali waliyoyafanya. Mwanafunzi atunge sentensi sahihi kama hizi:***

1) Kila mwanafunzi katika kundi lake alitoa ***mchango*** wake kwa kujibu maswali mbalimbali.
2) Katika maisha ya kila siku ***elimu*** ni kitu muhimu sana.
3) Vijana ambao hutumia ***dawa za kulevya*** huharibu maisha yao.
4) Sehemu ya nyuma ya kichwa huitwa ***kisogo***.
5) Wazazi wana wajibu wa ***kulea*** watoto kwa kuwafundisha maadili mema.
6) Kiongozi wa shule ***aliwakaribisha*** wanafunzi alipofika shuleni.
7) Miongoni mwa wahusika wa mjadala kuna ***kiongozi*** ambaye kazi yake ni kuongoza washiriki.
8) Tabia ya ***uzinzi*** ni ya kupigwa marufuku katika jamii ya Wanyarwanda.
9) ***Ulevi*** huwafanya watu wawe maskini.
10) Mitihani ya ***serikali*** hutayarishiwa wanafunzi kila mwisho wa mwaka.

**Kazi ya 4:** ***Katika makundi ya wanafunzi wanne wanne, mkufunzi awaombe wanafunzi kuambatanisha maneno yaliyoko katika orodha A na maelezo yaliyo katika orodha B. Mkufunzi atathmini kazi walizozifanya wanafunzi katika makundi. Yafuatayo ni majibu:***

| | | |
|---|---|---|
| 1) (j) | 5) (h) | 9) (d) |
| 2) (a) | 6) (i) | 10) ( c) |
| 3) (f) | 7) (b) | 11) (e) |
| 4) (i) | 8) (d) | |

**Sarufi: Matumizi ya viambishi rejeshi kulingana na ngeli za majina**

**Kazi ya 5:**

1) Asiyekuwepo na lake halipo.
2) Ngoma ivumayo ndiyo ya kupasuka.
3) Akufaaye kwa dhiki ndiye rafiki yako.
4) Zimwi likujualo halikukuli likakumaliza.
5) Wageni wafikao sasa ndio wetu.

**Matumizi ya Lugha: Maandalizi na utekelezaji wa mjadala**

**Kazi ya 6*: Zoezi hili lifanyiwe katika makundi ya wanafunzi watatu watatu. Wanafunzi wasome maelezo kuhusu mjadala kisha wajibu maswali yaliyopendekezwa. Mwalimu awaongoze wanafunzi kusoma maelezo yaliyomo vitabuni mwao. Mwalimu ahakikishe kuwa kila mwanafunzi alisoma maelezo yenyewe. Mwalimu asasihishe majibu yao. Majibu yaliyopendekezwa*:***

1) Mjadala ni mazugumzo ambayo yanaweza kufanyika katika makundi madogo au makubwa juu ya jambo fulani maalumu na ambayo yanaweza kuongozwa na mtu mmoja au watu wawili ambao wanazusha mawazo na kuhakikisha ikiwa kuna mwenendo mwema kati ya washiriki wa mazungumzo hayo.
2) Wanaoshiriki katika mjadala ni kiongozi wa mjadala, yeye anatoa muhtasari wa mawazo yaliyotolewa katika mjadala. Washiriki (hadhira) ambao hutoa hoja zao, wanaweza kuunga mkono maoni ya wenzao au kuyapinga kwa minajili ya kutoa michango yao ya kutatua tatizo linalojadiliwa.
3) Mambo ya kuzingatia katika uandalizi wa mjadala:
    - Kutumia vizuri muda uliopangwa: lazima kutumia muda vizuri kwa sababu kila mtu anaruhusiwa kutoa hoja yake.
    - Kuepuka na fujo na kelele: kelele huwafanya watu waliohudhuria mawasiliaono wasielewane ipasavyo.
    - Kupaza sauti unapotoa hoja kuhusu mada: anayezungumza anatakiwa kupaza sauti ili asikike na kila mtu aliyehudhuria. Hoja anazotoa huhitajika na kila mshiriki.
    - Kutoa maoni kwa madhumuni ya kutimiza lengo la mjadala: katika mjadala, kila mshiriki anahitajiwa kutoa maoni yatakayoangazia wengine kutoa maoni yao.

- Kutumia lugha isiyo ya matusi: matumizi mazuri ya lugha huwa njia mojawapo wa kuheshimia katika majadiliano. Lugha ya matusi hukasilisha wanataka kutoa hoja zao.
- Kuwaheshimu wengine: heshima ni kitu muhimu katika maisha ya kila mtu, katika mjadala lazima kuheshimiana na kusaidiana ipasavyo ili wawe na mwenendo sawa.
- Kupanga mawazo yako kabla ya kupata fursa: ni lazima kupanga mawazo kabla ya kupewa fursa ya kuzungumza ili utumie muda ipasavyo na lugha inayoeleweka.

**Kusikiliza na Kuzungumza**

**Kazi ya 7:** ***Zoezi hili ni la makundi. Wanafunzi wachague mada katika makundi yao kisha wawasilishe waliyoyazungumzia. Mkufunzi ahakikishe kwamba mwanafunzi kutoka kila kikundi anawasilisha hoja zake mbele ya darasa huku akirekebisha penye makosa.***

**Kuandika: Utungaji**

**Kazi ya 8:** ***Zoezi hili lifanywe na kila mwanafunzi binafsi. Wanafunzi waandike kifungu kwa kufuata kanuni walizopewa katika kitabu cha mwanafunzi na baadaye mkufunzi awaongoze na arekebishe kazi zao.***

## 4.6. Kazi ya utafiti

Katika mapumziko yako ya mwisho wa juma chunguzeni jinsi mijadala inavyofanyika katika sehemu mnazoishi na elezeni namana inavyosaidia kusuluhisha matatizo ya kijamii.

## 4.7. Muhtasari wa mada

Mada hii ya nne **"Mijadala"** ina masomo makuu **mawili** yanayohusiana na mada husika. Kila somo lina vipengele vidogo kama vile: kifungu cha habari, maswali ya ufahamu, matumizi ya msamiati, sarufi, matumizi ya lugha, maelezo muhimu, kusikiliza na kuzungumza na utungaji. Somo la kwanza linaeleza "**maana ya mjadala,"** umuhimu wake kwa wanafunzi, tabia zinazotarajiwa kwa washiriki wa **mjadala** na Matumizi ya viambishi rejeshi kulingana na ngeli za majina. Somo la pili linaeleza maandalizi na utekelezaji wa mjadala na matumizi ya viambishi rejeshi kulingana na ngeli za majina.

## 4.8. Maelezo ya ziada kwa mkufunzi

Sehemu hii inahusu maelezo ya ziada kwa mkufunzi. Sehemu hii inamsaidia mkufunzi kuwa na ujuzi wa kutosha kuhusu mada. Mkufunzi atoe kazi kwa wanafunzi katika makundi ya wanafunzi darasani, kisha atatoa kazi za nyumbani kwa kila mwanafunzi ambazo zitawasilishwa shuleni ili kupima uelewa wao

endapo darasani kutakuwepo na wanafunzi wasiojiweza kimasomo, mkufunzi ajaribu kuwasaidia li waweze kwenda sambamba na wenzao. Kwa wale wanafunzi wenye uwezo wa kuelewa zaidi kuliko wenzao wapewe mazoezi ya ziada darasani wakati mkufunzi akiendelea kuwasaidia wale wasiojiweza.

## 4.9. Tathmini ya mada ya nne

### *1) Uhusiano kati ya mjadala na mdahalo*

- Mjadala na mdahalo huhusisha watu wengi wanaojadiliana kuhusu jambo fulani.
- Katika mjadala na mdahalo kuna mada ambayo hutolewa mawazo, na mada hiyo ndiyo ambayo inamulikia mjadala na mdahalo.
- Katika mdahalo na mjadala kuna kiongozi ambaye kazi yake ni kuwasaidia wasemaji kutokiuka mada.
- Mdahalo na mjadala huwa na malengo sawa ya:

  Kukuza uwezo wa kitaaluma na hali ya udadisi kwa washiriki wa mjadala na mdahalo,

  Kukuza uwezo wa kushawishi watu hadharani ili wakubaliane na mawazo ya msemaji kuhusu jambo fulani,

  Kumwezesha mtu kupanga mawazo yake kwa mfuatano mzuri wakati anapoandika insha au habari,

  Kumwezesha mtu kutambua kipaji alicho nacho cha kuzungumza bila aibu mbele ya hadhira,

  Kukuza stadi ya utumiaji wa lugha kwa kutumia msamiati na matamshi bora ya lugha,

  Kumzoeza mtu kusikiliza na kupinga au kutetea maoni na hoja za wengine,

  Kuwapa watu wasaa wa kuelewana na wengine kutoka maeneo mbalimbali.

***Tofauti kati ya mdahalo na mjadala ni hizi zifuatazo:***

- Tofauti ya kwanza kati ya mdahalo na mjadala ni wahusika. Katika mdahalo kuna mwenyekiti, katibu, wasemaji wakuu wa upande wa utetetezi na upinzani na hadhira lakini kwenye mjadalo kuna kiongozi na hadhira tu,
- Katika mdahalo kuna wasemaji wakuu wanaotetea au wasiokubaliana na mada lakini kwenye mjadala kila yeyote anayetaka kutoa hoja anaruhusiwa na kiongozi,

- Kwenye mdahalo kuna pande mbili yaani upande wa utetezi na wa upinzani lakini kwenye mjadala hakuna makundi ya utetezi na upinzani,
- Mdahalo ni mashindano na mwishoni mwake washindi hupigiwa makofi lakini kwenye mjadala hakuna washindi; kiongozi wa mjadala anatoa suluhisho kutokana na mawazo yaliyotolewa wakati mjadala si mashindano.

2) ***Mambo ya kuzingatia katika utekelezaji wa mjadala ni haya yafuatayo:***

- Kutumia vizuri muda uliopangwa,
- Kuepuka na fujo na kelele,
- Kupaza sauti unapotoa maoni kuhusu mada,
- Kutoa maoni kwa madhumuni ya kutimiza lengo la mjadala,
- Kutumia lugha isiyo ya matusi,
- Kuwaheshimu wengine,
- Kupanga mawazo yako kabla ya kupata fursa,

3) ***Mambo ya kuepuka katika mdahalo ni kama haya yafuatayo:***

- Kupiga kelele,
- Kusababisha fujo,
- Kupoteza muda kwa bure,
- Kutumia lugha yenye matusi,
- Kutoheshimu wenzako,
- Kukejeli amri kutoka kwa mwenyekiti

4) ***Wanafunzi wachague mada moja, kisha waandae mdahalo wakisaidiwa na mkufunzi. Mkufunzi ahakikishe kwamba kila mwanafunzi anafanya mdahalo wake mwenyewe na baadaye wawasilishe mbele ya darasa.***

a) Wakoloni walileta mabaya mengi kuliko mazuri.
b) Shule za mabweni ni bora kuliko shule za kutwa.
c) Uzuri wa mtu si urembo bali ni tabia.
d) Kutoa si utajiri bali ni moyo.

## 4.10. Kazi za ziada

### 4.10.1. Kazi za urekebishaji

Kamilisha sentensi zifuatazo kwa kutumia maneno yafuatayo: **uvivu, kutetea, madhara**, **mwenyekiti, kulevya**

a) Dawa za **kulevya** huangamiza maisha ya binadamu na nchi kwa ujumla.

b) Ulevi una **madhara** kwa kazi tunazofanya kwa kuendeleza nchi zetu.

c) Matokeo ya ulevi ni **uvivu**, kufukuzwa kazini, uzinifu, ukatili na mengineyo.

d) Mdahalo huhusika na **kutetea** au kupinga fikra za watu kulingana na mada inayohusika.

e) Mjadala unahusu mawasiliano kati ya watu juu ya mada fulani bila kuzingatia uchaguzi wa **mwenyekiti** na katibu.

### 4.10. 2. Kazi jumuishi

Fanya maandalizi ya mjadala kwa kutoa mambo yanayoweza kuzingatiwa kuhusu mada hii :

- Kilimo bila mbolea ni kasoro kwa maendeleo ya jamii.
- Elimu bora ni nguzo muhimu kwa maendeleo ya taifa.

### 4.10.3. Kazi za nyongeza

Fanya kazi zifuatazo kuhusu mjadala.

a) Andaa mjadala kuhusu moja ya mada zifuatazo:

i) Ufugaji ni bora kuliko kilimo katika maendeleo ya jamii.

ii) Maendeleo ya jamii huchochewa na elimu bila ubaguzi.

# MADA YA 5

# UTUNGAJI WA INSHA ZA MASIMULIZI

## 5.1. Uwezo upatikanao katika mada

Kutunga insha fupifupi za masimulizi kwa kuzingatia kanuni za utungaji.

## 5.2. Ujuzi wa awali

Wanafunzi walisoma kuhusu utungaji wa insha za masimulizi katika kidato cha tatu cha shule za upili.Walisoma pia kuhusu alama za vituo katika kidato cha pili katika shule hizo za upili. Somo hili ni maendeleo ya masomo hayo waliyoyasoma lakini hili ni la kiwango cha juu kulingana na yale ya awali.

## 5.3. Kuingizwa kwa masuala mtambuka katika mada

Mada hii ina somo moja. Mkufunzi ataingiza masuala mtambuka katika kufundisha na hata katika kazi zote zitakazofanywa na wanafunzi kama ifuatavyo:

- **Mafunzo kuhusu amani na maadili.**

  Utungaji wa insha fupifupi na sentensi zitakazotumiwa katika kutumia vizuri alama za vituo ziwe na mwelekeo wa kuimarisha amani na maadili. Kwa kutunga sentensi, mkufunzi awaongoze wanafunzi kutunga sentensi zenye mafunzo yanayohusu amani na maadili. Ni kusema kwamba malengo ya utungaji wowote na kazi zozote za kitabuni pamoja na zile za nje ya kitabu kama vile darasani na mahali pengine ambapo somo linaweza kufundishiwa yatahusu kuimarisha amani na maadili katika jamii.

- **Elimu isiyo na ubaguzi**

  Makundi yote ya wanafunzi katika kufanya kazi yoyote ya somo hili yanatarajiwa kujumuisha wanafunzi bila ubaguzi wowote. Hii ina maana ya kwamba wanafunzi wenye matatizo fulani kama yale ya kutoona, kutosikia vizuri, kutembea vigumu na mengineyo watafanya kazi pamoja na wanafunzi wengine. Mkufunzi ahakikishe kwamba hatawasimanga au kuwakashifu wenye matatizo tofauti, bali atawashirikisha kufanya iwezekanavyo ili waendelee na masomo kama wanafunzi wenzao.

- **Usawa wa jinsia**

  Kwa kuchanganya wanafunzi katika jozi na makundi mbalimbali ya kazi, mkufunzi ahakikishe ya kwamba wavulana na wasichana wanafanya kazi kwa pamoja bila ubaguzi wowote wa kijinsia. Lugha itakayotumiwa darasani isibague wanafunzi kijinsia ili wote wajisikie sawa katika masomo yao.

## 5.4. Mwongozo kuhusu kazi ya utangulizi wa mada

Kwa kutangulia mada, mkufunzi aulize maswali ambayo yatawasaidia wanafunzi kufunua mada hii. Mkufunzi aulize wanafunzi kuhusu mambo wanayokumbuka kuhusu utungaji wa insha hasa hasa insha za masimulizi. Awaulize pia kuhusu matumizi sahihi ya alama za vituo ambazo walisoma katika shule za sekondari, kiwango cha kwanza.

## 5.5. Orodha ya masomo na tathmini

| | | | |
|---|---|---|---|
| | **Kichwa cha somo** | **Malengo ya kujifunza (kutoka muhtasari: maarifa na ufahamu, stadi na maadili na mwenendo mwema)** | **Idadi ya vipindi** |
| | **Utungaji wa insha za masimulizi** | **Maarifa na ufahamu:**<br>- Kutoa maana ya insha za masimulizi na kutaja sehemu kuu zake<br>- Kuonyesha sifa za aya<br>- Kutoa aina mbalimbali za insha na kuzieleza<br>- Kutaja aina ya alama za vituo na kueleza matumizi yake.<br>**Stadi:**<br>- Kuchunguza kiini cha mada<br>- Kukusanya hoja kuhusu mada husika na kuzipanga kwa mfuatano mzuri<br>- Kuchunguza sifa za sehemu kuu za insha<br>- Kutunga insha za masimulizi kulingana na mada husika<br>- Kutumia kwa usahihi alama za vituo katika uandishi wa insha za masimulizi<br>- Kubainisha sehemu kuu na mawazo muhimu katika insha iliyotungwa | **5** |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1 | | - Kusimulia hadharani kiini cha insha iliyotungwa.<br><br>**Maadili na mwenendo mwema:**<br>- Kukuza tabia ya kuhifadhi mazingira<br>- Kukuza tabia ya kuheshimu watu kwa kuendeleza usawa wa jinsia katika jamii<br>- Kukuza na kuendeleza tabia ya kujieleza na kuonyesha msimamo wake kuhusu masuala yaliyopo<br>- Kudumisha mshikamano na ushirikiano katika jamii kupitia utunzi wa insha za masimulizi na maelezo<br>- Kuonyesha mwenendo wa kuimarisha amani na maadili | |
| **Tathmini ya mada** | | | 2 |
| **Idadi kamili ya vipindi** | | | 7 |

# SOMO LA 7: UTUNGAJI WA INSHA ZA MASIMULIZI

## a) Malengo ya ujifunzaji

- Kutoa maana ya insha za masimulizi na kutaja sehemu kuu zake
- Kuonyesha sifa za aya
- Kutoa aina mbalimbali za insha na kuzieleza
- Kutaja aina ya alama za vituo na kueleza matumizi yake.
- Kukusanya hoja kuhusu mada husika na kuzipanga kwa mfuatano mzuri
- Kutunga insha za masimulizi kulingana na mada husika
- Kutumia kwa usahihi alama za vituo katika uandishi wa insha za masimulizi
- Kusimulia hadharani kiini cha insha iliyotungwa.
- Kukuza na kuendeleza tabia ya kujieleza na kuonyesha msimamo wake kuhusu masuala yaliyopo
- Kudumisha mshikamano na ushirikiano katika jamii kupitia utunzi wa insha za masimulizi na maelezo.

## b) Zana au vifaa vya ufundishaji

Ili somo liweze kufika kwenye malengo yake, ni lazima mkufunzi ajaribu kutafuta zana za ufundishaji zitakazomsaidia kufanikisha somo lake ili kukidhi mahitaji ya wanafunzi na malengo ya somo husika.

Katika somo hili zana muhimu ni: Kitabu cha mwanafunzi, mwongozo wa mkufunzi, vinasa sauti, kamusi ya Kiswahili sanifu, ubao, chaki na vifaa vinavyoweza kuwasaidia wanafunzi kuelewa somo akifuatilia kwa karibu mkazo juu ya hali za wanafunzi wanaohitaji uangalifu maalumu kama wale wenye shida tofauti. Anaweza kutumia vifaa tofauti vya teknolojia kama vile tarakilishi, projekta na vifaa vingine vinavyoweza kupatikana.

## c) Ujuzi wa awali/Marudio/Utangulizi

Mkufunzi aulize wanafunzi maswali kuhusu matumizi sahihi ya alama tofauti. Anaweza pia kuwaomba kutunga sentensi mbalimbali kufuatana na alama za vituo anazowapa. Awaulize pia kuhusu utungaji wa insha kwa ujumla na insha za masimulizi ili aweze kujua kwa ukweli ujuzi walio nao kuhusu utungaji wa insha.

**d) Maelekezo kuhusu kazi za ujifunzaji**

Katika hatua hii, mkufunzi atafute mbinu mbalimbali zitakazomwezesha kufika kwenye malengo ya somo lake. Katika somo hili mkufunzi atilie mkazo mambo yafuatayo:

- **Utumiaji wa makundi ya wanafunzi**: Mkufunzi aweke wanafunzi katika makundi ya watu wawili, watatu, wanne au zaidi kulingana na idadi kamili ya wanafunzi darasani. Wanafunzi wakishiriki katika kutoa mchango wao kwa kujibu maswali wanayopewa. Mkufunzi achunguze kwa makini namna kazi inavyofanyika katika makundi kwa kutumia muda vizuri na kutoa msaada ikiwa unahitajika.
- **Kazi binafsi kwa mwanafunzi**: Kwa kusaidia kila mwanafunzi na kuhakikisha kwamba lengo la somo limetimizwa, mkufunzi awape wanafunzi kazi ya binafsi. Kila mwanafunzi ajibu maswali peke yake bila msaada wa mkufunzi au mwanafunzi mwenzake.
- **Mihadhara**: Mkufunzi atumie njia hii kwa kuwapa wanafunzi fursa ya kutumia lugha. Wanafunzi wajitokeze mbele ya wenzao ili kutoa maelezo yao kuhusu mada husika. Maswali ya wanafunzi yajibiwe na wanafunzi wenzao kadiri iwezekanavyo. Mkufunzi aongoze mihadhara hii na kuhakikisha kwamba wanafunzi wote wanashirikia kutega sikio na kuuliza maswali. Mkufunzi ajibu maswali ambayo wanafunzi wote wanashindwa kujibu.
- **Maelezo ya Mkufunzi**: Mkufunzi kwa ujuzi wake ahakikishe kwamba maelezo anayotoa yanawawezesha wanafunzi kuelewa somo wanalojifunza. Ikiwa mkufunzi anatambua kasoro fulani, ni lazima awaelezee wanafunzi vya kutosha akisisitizia kasoro aliyoitambua.

**e) Majibu:**

Yafuatayo ni majibu ya maswali ambayo yanatarajiwa kutolewa na wanafunzi katika somo hili.

**Kidokezo:** Wanafunzi wataangalia mchoro na kuzungumzia vile wanavyoona. Mkufunzi atawaelekeza wanafunzi katika ugunduzi huo.

**Kusona na ufahamu: Mafanikio ya kudumu**

**Kazi ya 1:** ***Mkufunzi anawaomba wanafunzi katika makundi kujibu maswali ya ufahamu. Yafuatayo ni majibu:***

1) Masengesho alipokuwa mtoto mdogo hakubahatika kulelewa na wazazi wake kwani walifariki angali mdogo akachukuliwa na kulelewa na shangazi yake.

2) Masengesho alipewa zawadi nyingi baada ya kumaliza masomo yake ya shule za Sekondari Masengesho kwa kuwa alipata cheti kilichokuwa na alama nzuri. Jambo hili liliwafurahisha watu wengi: walimu na majirani zake. Wengi waliompongeza siku hiyo walimletea zawadi nyingi.

3) Masomo ya muda mfupi aliyoyafuata yalihusu kuandaa miradi midogo midogo ya kujiendeleza na jinsi ya kuifanikisha.

4) Masengesho alipewa tuzo kwa kubadilisha maisha ya watu wengi. Alitengeneza ajira kwa watu wengi.

5) Ndiyo ninapata funzo kwa kifungu hiki kama vile:

- Kuwa mwanafunzi au mfanyakazi mwenye bidii.
- Kutokata tamaa.
- Kuwa na malengo au mipango maishani mwa mutu.
- Kuwa mtu mwenye mawazo na mitazamo imara wa maisha.
- Somo la kufanya mambo mengi kwa muda mfupi na kwa ukamilifu, n.k.

6) Maana ya methali ni hizi zifuatazo:

**a) Mvumilivu hula mbivu**: Wazazi wake Masengesho walifariki angali mdogo akachukuliwa na kulelewa na shangazi yake. Baada ya kifo cha mama yake alivumilia maisha ya kuwa yatima kwa wazazi wote baadaye akawa tajiri maarufu aliechangia kuyaboresha maisha ya majirani zao kwa kuwapatia kazi. Kuvumilia ni jambo muhimu katika kumsaidia mtu kuboresha hali ya maisha yake.

**b) Mchumia juani hulia kivulini:** Masengesho alikuwa mwanafunzi mwenye bidii tangu shule za chekechea hadi kiwango alichofikia. Masengesho alikuwa anatumia nguvu zake zote. Alifanya kazi ya ukalimani kwa bidii kiasi kwamba watalii wengi walifurahia huduma yake. Alikuwa msichana asiyekata tamaa na kila aliposhikilia hitaji lake alilifuatalia mpaka lilipokamilika. Aliandaa vizuri mradi wa kilimo na ufugaji, akajenga vibanda vya mifugo yake. Baadaye alikuwa alipata mali nyingi na kuanza kujulikana kote nchini kwa uwezo wake wa kufanya mambo mengi kwa muda mfupi na kwa ukamilifu. Serikali ilimpatia tuzo kwa watu waliochangia kubadilisha maisha ya watu wengine. Masengesho alikuwa miongoni mwa matajiri maarufu. Kwa machache, Masengesho alikula matunda kutokana na kazi aliyoifanya katika hali ngumu. Mtu anayefanya kazi ngumu hupata matunda mazuri baadaye.

**Msamiati kuhusu kifungu cha habari**

**Kazi ya 2: *Mkufunzi anawaomba katika makundi ya wanafunzi wawili wawili kutumia Kamusi ya Kiswahili Sanifu katika kutunga sentensi sahihi kwa kutumia maneno waliyopewa. Yafuatayo ni majibu:***

1) **Mafanikio:** Watu wengi wanafanya kazi zao lakini mafanikio yao ndiyo huonyesha tofauti ya mazao ya kazi hizo.
2) **Akaunti:** Jirani yangu alifungua akaunti katika benki "Songa mbele" ili apate mkopo wa kumsaidia kufanya biashara.
3) **Tafrija:** Watu walikuwa wengi katika tafrija ya ndoa ya kaka yangu.
4) **Mradi:** Ninataka mradi wa kufuga kuku za kutaga mayai.
5) **Kukata tamaa:** Yule kijana alifaidika katika maisha yake kwa kuwa wazazi wake walimuunga mkono badala ya kumkata tamaa.

**Kazi ya 3: *Mkufunzi anaomba kila mwanafunzi kuhusisha maneno kutoka sehemu A na maana yake kwenye sehemu B.***

**Masahihisho:**

| **Sehemu A** | **Sehemu B** |
|---|---|
| **1. Mkalimani** | f. Mtu afasiriye papo kwa papo mazungumzo kutoka lugha moja kwenda lugha nyingine. |
| **2. Utalii** | j. Hali ya kusafiri mbali au kuvinjari huku na huko ili kuyafurahia mandhari. |
| **3. Shahada** | h. Cheti au karatasi maalumu anayopewa mtu baada ya kupata mafunzo fulani katika chuo. |
| **4. Mshahara** | Malipo ya mwezi anayopewa mwajiriwa kwa kazi aliyofanya; janguo. |
| **5. Yatima** | i. Mtoto ambaye mzazi wake au wazazi wote wamekufa. |
| **6. Stashahada** | b. Cheti maalumu chenye hadhi ya chini kuliko shahada. |
| **7. Mtaji** | c. Mali inayotumika kuanzishia au kupanulia biashara au shughuli yoyote ya kuzalisha mali. |
| **8. Mwaliko** | e. Mwito wa kumtaka mtu au watu kuhudhuria mahali. |
| **9. Tabia** | d. Matendo ambayo mtu amezoea kuyafanya mara kwa mara;mwenendo;mazoea; desturi. |
| **10. Kudumu** | g. Kuendelea kuishi au kuwepo kwa muda wote. |

**Sarufi kuhusu matumizi ya alama za vituo au uakifishaji**

**Kazi ya 4:** ***Chunguza sentensi ambazo zinafuata na kujadili na mwenzako unavyoziona:***

1) Ehee! Kumbe yeye ni mwizi!
2) Mwalimu wa Mitaala wa shule letu ni mtu mpole kabisa.
3) Ninaenda sokoni kununua vitu vingi: maembe, mapapai, machungwa, madaftari, kalamu na kuku.
4) Nyinyi mnaona vipsi siku za leo?
5) Masomo haya si ya kukuangamiza; masomo haya ni ya kuboresha hali ya maisha yako.

**Maelezo:**

Ndani ya sentenzi hizi kuna matumizi ya alama za vituo mbalimbali kulingana na maumbile ya kila sentensi. Kuna alama ya kushangaa, alama ya nukta au kituo, alama ya nukta mbili, alama ya mkato wa chini au koma, alama ya kuuliza au kiulizi pamoja na alama ya nukta na mkato.

**Matumizi ya lugha**

**Kazi ya 5:** ***Alama za vituo katika dondoo hii zingewekwa kama hivi:***

Hmm**!** Unataka nikuambie sifa za mtu ninayempenda**?** Bila shaka ninampenda sana baba**.** Baba yangu anaitwa John Mugabo**.** Yeye ni mrefu na mweupe**.** Baba ana macho mazuri na nywele nyingi nyeusi kichwani**.** Yeye hupenda kuvalia mavazi tofauti**:** suti**,** kanzu**,** mashati meupe na suruali nyeusi kila wakati**,** isipokuwa Jumamosi tunapoenda kucheza kandanda naye**.** Baba ni mchezaji hodari sana katika kandanda na yeye hufurahia sana mchezo huu**.** Baba yangu ni mwalimu mkuu katika shule ya sekondari ya Kigali**.** Anaheshimiwa sana na walimu wote**,** wanafunzi hata na wazazi**.** Sifa zake nzuri ndizo humfanya baba apendwe na kila mtu**.**

**Kazi ya 6:** ***Majibu ni yafuatayo:***

1) Utangulizi mzuri ni muhimu katika insha kwa sababu ndio hudondoa kwa ufupi kabisa kile kinachoelezwa kwenye insha.
2) Insha ya masimulizi huwa na utangulizi ambao ni sehemu ya mwanzo yenye urefu usiozidi aya moja. Utangulizi hudondoa kwa ufupi kabisa kile kinachoelezwa kwenye insha.

Kiini cha insha ya masimulizi ni sehemu tunayoweza kusema kwamba ni insha yenyewe. Kwenye kiini ndipo ufafanuzi wote hutolewa. Ufafanuzi huu hupangwa katika aya moja au zaidi. Hapa ndipo mwandishi hubainisha mawazo yake, huthibitisha, hushawishi, huhimiza na hufafanua. Baada ya kiini huja hitimisho, yaani sehemu ya mwisho wa insha ya masimulizi ambayo haizidi aya moja. Katika sehemu hii, mwandishi anaweza kurejea kwa ufupi sana yale aliyozungumzia kwenye insha yake. Anaweza kuonyesha msimamo wake, anaweza kutoa mapendekezo, au kuwahimiza walengwa wake kuchukua hatua fulani.

3) Katika kuandika insha ya masimulizi, mwandishi atazingatia mambo haya: Atabaini ni mada gani ya kuandikia na kuielewa vema. Atapanga mawazo katika mtiririko wenye mantiki, atatumia mtindo unaoendana na kusudi la insha ya masimulizi. Kwa mfano, mtindo wa masimulizi unafaa kwa hadithi au insha nyingine za kisanaa. Atatumia lugha fasaha na inayoeleweka, atafuata kanuni za uandishi, kwa mfano matumizi ya alama za uandishi, aya, herufi kubwa na herufi ndogo. Mwandishi atapanga insha katika muundo wake, yaani kichwa, utangulizi, kiini na hitimisho.

**Kusikiliza na kuzungumza**

**Kazi ya 7:** ***Majibu ni yafuatayo:***

1) Katika utungaji wa insha kuna insha za masimulizi, insha za wasifu, insha za picha, insha za mdokezo, insha za methali, insha za hoja na insha za kubuni.

2) Kifungu kuhusu Masengesho ni insha ya masimulizi. Kwa sababu insha nzima inasimulia maisha yake Masengesho kimaalum au kiukweli.

3) Tofauti iliyoko baina ya insha ya wasifu na insha ya masimulizi ni kwamba insha za masimulizi ni insha ambazo ndani yake mwandishi anasimulia au anaeleza tukio fulani maalum la kweli kwa njia ya kisanaa, ambapo insha za wasifu ni ambazo hueleza sifa za mtu, kitu au jambo fulani.

4) Mara zote mwandishi wa insha ya methali hulazimishwa kutetea methali aliyopewa kwa sababu mada yake huwa ni methali ambayo mwandishi anapaswa kujadilia.

**Kuandika kuhusu utungaji wa insha ya masimulizi**

**Kazi ya 8:** ***Mwelekeo wa jibu:***

**Mada:** Rafiki yako anayesoma katika kidato cha tano amefukuzwa shuleni kwa sababu anatumia dawa za kulevya na kushiriki ulevi. Simulia kilichoendelea.

Mwanafunzi atakuwa na uhuru wa kuendeleza insha kwa kuhakikisha kwamba insha yake ni ya masimulizi, pamoja na kuhakikisha kwamba anafuata uandishi mzuri wa aya n ahata uandishi wa insha ya masimulizi. Matumizi ya alama za vituo yanatarajiwa kuwa sahihi kama ilivyo katika insha yoyote ile.

**Atazingatia mambo haya:**

- Insha yenye sehemu tatu: utangulizi, kiini na hitimisho.
- Kupanga mawazo katika mtiririko wenye mantiki.
- Kutumia msamiati mwafaka kwa kutegemea mada.
- Maelezo yote yatolewe kwa undani.
- Maelezo yatolewe kwa njia ya kuvutia.
- Kutumia vizuri sarufi na alama za uakifishaji, n.k

## 5.6. Kazi ya utafiti

Wanafunzi wapewe kazi ya utafiti kuhusu aina za insha na sifa za aya ya insha. Baada ya kufanya kazi hii wawasilishe matokeo ya utafiti wao darasani.

## 5.7. Muhtasari wa mada

Mada hii ya tano **"Utungaji wa insha za masimulizi"** ina somo moja. Somo hili lina vipengele vidogo kama vile: kifungu cha habari, maswali ya ufahamu, matumizi ya msamiati, sarufi kuhusu matumizi ya alama za vituo, matumizi ya lugha, kusikiliza na kuzungumza, kuandika, pamoja na na maelezo muhimu. Somo hili linazungumzia pia sehemu za insha pamoja na aina mbalimbali za insha. Mwisho wake kuna tathmini ya mada kwa ujumla.

## 5.8. Maelezo ya ziada kwa mkufunzi

Sehemu hii inahusu maelezo ya ziada kwa mkufunzi. Sehemu hii inamsaidia mkufunzi kuwa na ujuzi wa kutosha kuhusu mada na jinsi ya kuendeleza ufundishaji wake. Kwa kufundisha mada hii, yeye ana uhuru wa kutumia matini yingine anazoona kuwa ni muhimu ili kufanikisha malengo ya somo husika.

## 5.9. Tathmini ya mada

1) Insha za masimulizi ni aina ya insha ambazo ndani yake mwandishi anasimulia au anaeleza tukio fulani maalum la kweli kwa njia ya kisanaa.

2) Sehemu za insha ya masimulizi ni kichwa ambacho ni mada ya insha au kinachozungumziwa. Kichwa hakipaswi kuwa na maneno mengi. Utangulizi ni sehemu inayotanguliza insha. Huwa na aya moja ambayo haina mistari mingi. Hupaswa kuwa na mvuto kwa msomaji na kutoa mwelekezo wa insha yenyewe. Mwili au sehemu kuu ndiyo hasa insha yenyewe. Mwili wa insha ya masimulizi huundwa na aya zinazoendeleza mada yake. Kila aya lazimza ichangie katika kuliendeleza wazo kuu. Ni vyema kuhakikisha kuwa kuna muungano ulio wazi kutoka aya moja hadi nyingine. Hitimisho pia ni sehemu ya mwisho wa insha. Katika sehemu hii mwandishi hurudilia kwa ufupi yale aliyoyaelezea katika insha yenyewe.

3) Aina za insha za masimulizi, insha za wasifu, insha za picha, insha za mdokezo, insha za methali, insha za hoja na insha za kubuni.

4) Alama za vituo kwenye sentensi hizi zinaweza kuwekwa kama ifuatavyo:

   a) Afanaalek**!** Kumbe nimesahau kuwa leo ni siku yangu ya kuzaliwa**!**

   b) Wanafunzi wa kidato cha tano wanakosa miaka mingapi kumalizia shule za upili**?**

   c) Niletee kwenye ofisi yangu vyombo vifuatavyo**:** kalamu**,** karatasi**,** meza**,** viti**,** deski na makabati**.**

   d) Mwalimu alisema**, "**Fanyeni kazi hii katika dakika arobaini tu**."**

   e) Watu wote **(**wanaume na wanawake**)** watashiriki katika mkutano wa kijiji chetu**.**

5) Katika kutunga insha ya masimulizi kuhusu shule yake, mwanafunzi anatakikana kusimulia juu ya shule yake. Atahakikisha kwamba anatumia vizuri alama za vituo. Mwanafunzi atatoa maelezo bila ya kuacha mambo yoyote muhimu. Maelezo yawe yanalenga kufunua milango yote ya hisia za msomaji, hususani kuona, kusikia, kugusa, kuonja na kunusa iwezekanavyo. Ataeleza mambo kwa ukweli katika kutoa picha iyayokusudiwa kumfikia msomaji. Apange maelezo katika mtiririko mzuri ulio na mantiki. Insha iwe na mshikamano aya kwa aya.

## 5.10. Kazi za ziada

### 5.10.1. Kazi za urekebishaji

Mapendekezo ya maswali na majibu ya kuwasaidia wanafunzi wenye kipaji cha hali ya chini.

1) Taja sehemu za insha ya masimulizi.

2) Andika aina za insha za masimulizi.

3) Weka alama za vituo kwenye sentensi ambazo zinafuata:

a) Watoto wanakaa chini na kutulia hivi wakiangalia filamu

b) Kumbe alikuwa mwizi wa siku nyingi

**Mapendekezo ya majibu:**

1) Sehemu za insha ya masimulizi ni: Kichwa cha habari, utangulizi, kiini cha insha na hitimisho.

2) Aina za insha za masimulizi ni: Insha za masimulizi, insha za wasifu, insha za picha, insha za mdokezo, insha za methali, insha za hoja na insha za kubuni.

3) a) Watoto wanakaa chini na kutulia hivi wakiangalia filamu.

b) Kumbe alikuwa mwizi wa siku nyingi!

### 5.10.2. Kazi jumuishi

1) Taja sehemu za insha ya masimulizi kisha ueleze kila sehemu.

2) Tunga sentensi zako mwenyewe ambazo zina alama za vituo zinazofuata:

a) Alama ya mkato wa chini (koma).

b) Alama ya kushangaa.

c) Alama ya kituo (nukta).

d) Alama ya nukta mbili.

**Majibu yaliyopendekezwa:**

1) Sehemu za insha ya masimulizi na maelezo ya kila sehemu.

a) Kichwa cha habari cha insha: Kichwa hiki huwa ni maneno machache, takribani matano, ambayo ndiyo jina la insha. Kichwa cha habari huandikwa juu, katikati kwenye ukurasa wa kwanza wa insha. Mara nyingi, huandikwa kwa herufi kubwa na hubeba wazo kuu la insha.

b) Utangulizi: Hii ni sehemu ya mwanzo yenye urefu usiozidi aya moja. Utangulizi hudondoa kwa ufupi kabisa kile kinachoelezwa kwenye insha.

c) Kiini cha insha: Hii ni sehemu tunayoweza kusema kwamba ni insha yenyewe. Kwenye kiini ndipo ufafanuzi wote hutolewa. Ufafanuzi huu hupangwa katika aya moja au zaidi. Hapa ndipo mwandishi hubainisha mawazo yake, huthibitisha, hushawishi, huhimiza na hufafanua.

d) Hitimisho: Hii ni sehemu ya mwisho wa insha ya masimulizi ambayo haizidi aya moja. Katika sehemu hii, mwandishi anaweza kurejelea kwa ufupi sana yale aliyoyazungumzia katika insha yake. Anaweza

kuonyesha msimamo wake, anaweza kutoa mapendekezo au kuwahimiza walengwa wake kuchukua hatua fulani.

2. a) Nimenunua kalamu, daftari na chaki.
   b) Moyo ulidunda ndu! ndu!
   c) Kazi hii ilikuwa rahisi kwangu.
   d) Kuna aina kadhaa za vivumishi: vivumishi vya sifa, vivumishi vya idadi, vivumishi viwakilishi na kadhalika.

### 5.10.3. Kazi za nyongeza:

Mapendekezo ya maswali na majibu kwa wanafunzi wenye kipaji cha hali ya juu.

**Maswali:**

1) Taja alama za vituo tano, toa maelezo kuhusu matumizi ya vituo hivyo kisha utoe mfano wa sentensi kwa kila alama.

**Majibu:**

a) Nukta: Hutumiwa kuonyesha mwisho wa sentensi.

   **Mfano:** Mimi ni mwanafunzi.

b) Mkato au koma: Hutumiwa kuonyesha orodha ya vitu.

   **Mfano:** Ninakwenda sokoni kununua maharage, mahindi, viazi vitamu na viazi mviringo.

c) Alama ya kuuliza: Hutumika kuuliza swali.

   **Mfano:** Je, umefika nyumbani ?

d) Matumizi ya nuktambili: Kuonyesha mwanzo wa orodha.

   **Mfano:** Kanyange anahitaji vifaa vifuatavyo: Rula, karatasi na kalamu.

e) Mkwaju: Hutumiwa kuonyesha kuwa kitu mojawapo ya vitu vilivyotajwa kinaweza kutumiwa badala ya vingine.

   **Mfano:** Tarakilishi/Kompyuta imerahisisha jinsi kazi hufanywa siku hizi.

2) Tunga insha ya masimulizi kwenye ukurasa mmoja kuhusu mada unayojichagulia.

**Mwelekeo wa kujibu kazi hii:**

Mkufunzi akumbushe wanafunzi sehemu za insha na sifa za kila sehemu ili wazizingatie wakati wa kutunga insha walizojichagulia.

# Marejeo


1) Waititu, F. na Wenzake (2008). *Kiswahili Fasaha. Kitabu cha Mwanafunzi. Kidato cha Tatu*. Oxford University Press, East Africa Ltd, Nairobi, Kenya.

2) TUKI (2004). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu. Toleo la pili*. Oxford University Press.

3) Bakhressa, S.K. na Wenzake (2008). *Kiswahili Sanifu. Kitabu cha Mwanafunzi. Darasa la Saba*. Oxford University Press, East Africa Ltd, Elgon Road, Upper Hill, Nairobi, Kenya.

4) Nkwera, F.M.V. (1978). *Sarufi na Fasihi Sekondari na Vyuo*. Tanzania Publishing House, Dar Es Salaam.

5) HARERIMANA, F. (2017). *Tujivunie Lugha Yetu. Kitabu cha Mwanafunzi, Kidato cha 5*. MK Publishers (R) Ltd. Kigali, Rwanda.

6) Ndalu, A. E. (2016). *Masomo ya Kiswahili Sanifu. Kitabu cha Mwanafunzi. Kidato cha 2*. Moran (E.A) Publishers Limited.

7) Ntawiyanga, S. na Wenzake (2017). *Kiswahili kwa Shule za Rwanda. Mchepuo wa Lugha, Kidato cha 5*. Longhorn Publishers (Rwanda) Limited. Kigali, Rwanda.

8) Kenya Literature Bureau (2006). *Kiswahili kwa Darasa la Nane. Kitabu cha Wanafunzi*. Kenya Literature Bureau, Nairobi, Kenya.

9) Ntawiyanga, S. na Wenzake (2017). *Kiswahili kwa Shule za Rwanda. Mchepuo wa Lugha, Kidato cha 6*. Longhorn Publishers (Rwanda) Limited. Kigali, Rwanda.

10) Niyirora, E. & Ndayambaje, L. (2012): *Kiswahili Sanifu kwa Shule za Sekondari. Kitabu cha Mwanafunzi Kidato cha Tano*. Tan Prints (India) Pvt. Ltd.

11) *https://es-la.facebook.com/OfficialMindsetMCHealthForChangeClub/posts/madhara-ya-kutumia-simu-smartphone-kwa-muda-mrefu-kiafya-na-kijamiimatumizi-ya-s/705366649652166/*